IKULU

ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 012 ISSN 1821 - 8253 OKTOBA - DISEMBA 2013

Dk. Shein

ameuzindua rasmi Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Bodi ya Wahariri

Mhariri Mkuu
Hassan K. Hassan

Mhariri Msaidizi
Ali S. Hafidh

Waandishi
Said J.Ameir
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

Mpiga Picha
Ramadhan O. Abdalla

Msanifu
Aziz I. Suwed

UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Afisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.

Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.BOX: 2422

Zanzibar - Tanzania

Phone: +255 223 081/5

Fax: 024 223 3722

Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz

Maoni ya Mhariri

Amani na utulivu ndio misingi mikuu ya kiutawala

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein, imekuwa ikitekeleza kazi zake vizuri kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya 1984 na Sheria katika kuwatumikia wananchi, kama ilivyofafanuliwa katika katiba hiyo.

Imeelezwa kwenye katiba hiyo kifungu cha 9(2)(a) kuwa, mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali unatokana na wananchi wenyewe. Kwa hivyo, viongozi wa Serikali ya awamu ya saba kama walivyo viongozi wengine waliotangulia, wameingia madarakani wakifahamu wajibu wao wa kuwaletea maendeleo wananchi wote bila ya ubaguzi na kwamba Serikali iliyopo inawajibika kwao.

Kifungu cha 9(b) cha Katiba hiyo pia kinaeleza kuwa Usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndiyo lengo kubwa la Serikali. Hivyo, Serikali imekuwa ikiendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa usalama na utulivu wa nchi unakuwepo wakati wote, na mshikamano na mapenzi baina ya wananchi yanaendelezwa.

Suala hilo limekuwa likipewa umuhimu wa kipekee kwa kuamini kwamba amani na utulivu ndizo nguzo kubwa za maendeleo ya Zanzibar na ndiyo maana Serikali imekuwa na tahadhari kubwa juu ya usalama wa wananchi wake, na haisiti kuchukua hatua za kisheria inapobaini kuwa usalama, utulivu, amani na mshikamano wa Wazanzibari vinahatarishwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimeendelea kuchukua hatua zinazofaa bila ya kuwa na khofu wala woga, dhidi ya watu au makundi yenye kuhatarisha amani na usalama wa watu na taifa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Sambamba na hatua hiyo, viongozi wakuu wa Serikali na hasa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein mara kadhaa amekuwa akitoa wito kwa wananchi wote kuzidi kuimarisha umoja, amani na utulivu ili kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyopatikana yanakuwa endelevu.

Akizungumza na waandishi wa habari, miaka mitatu baada ya kuchaguliwa kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo kwa mara ya kwanza iko chini ya muundo wa Umoja wa Kitaifa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alielezea mafanikio makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yaliyopatikana katika kipindi hicho, ambacho baadhi ya watu walikuwa na wasi wasi wa mafanikio ya serikali hiyo.

Dk. Shein alitumia fursa hiyo kuelezea kwa takwimu mafanikio ya Serikali anayoiongoza katika kutekeleza ilani ya CCM katika sekta mbali mbali zikiwemo sekta za uchumi, huduma za jamii, miundombinu, utawala bora na nyinginezo kwa maendeleo ya Zanzibar.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu tokea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa kuingia madarakani, Zanzibar iko salama na wananchi wanaishi kwa amani, utulivu na mshikamano. Katika kipindi cha mwaka 2012 kwa nyakati tofauti wananchi walishuhudia vitendo vya vurugu na fujo, ambavyo vilikuwa vikifanywa na baadhi ya watu, lakini vitendo hivyo vilidhibitiwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Kwa kuwa jukumu la kuendeleza umoja, maendeleo ya watu na ustawi wa jamii katika nchi ni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali hiyo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita imekuwa ikiendelea kutoa huduma za kutosha kwa ajili ya kuendeleza watu katika njia za mtu kuwa huru kwenda atakapo na kutoa haki zote za kuishi kwa Wazanzibari bila ya ubaguzi.

Sambamba na hatua hizo, amesema Serikali imedhamiria kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa vyeo dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka, kusimamia maendeleo ya uchumi wa nchi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyowekwa na Katiba na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, kuratibu na kusimamia uendeshaji wa rasilimali muhimu za nchi.

Kimsingi mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi kifupi cha miaka mitatu, yanatokana na ushirikiano mkubwa wa wananchi kuiunga mkono serikali yao katika harakati mbali mbali za maendeleo ambazo zinaendelea kufanyika katika mazingira ya amani, utulivu na mshikamano.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi bahasha Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NSSF Chiku Matesa baada ya kuchangia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wakati wa sherehe ya uzinduzi wa Mfuko huo tarehe 21 Disemba, 2013

Dk. Shein ameuzindua rasmi Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amezindua Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kusema kuwa hatua hiyo ni muendelezo wa jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kutekeleza dhamira ya waasisi wa Mapinduzi ya mwaka 1964 ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Aliongeza kuwa mbali ya kutekeleza dhamira hiyo mfuko huo pia unakwenda sambamba na utekelezaji wa lengo la nne la MKUZA II la kuimarisha sekta binafsi lenye shabaha ya kuongeza upatikanaji wa mikopo kutoka asilimia 43.2 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 86.9 ifikapo mwaka 2015.

Mfuko huo wenye thamani ya shilingi 1.101 bilioni unatarajiwa kutoa mikopo kwa wananchi yakiwemo makundi mbalimbali likiwemo kundi la vijana waliomaliza masomo katika vyuo na skuli za sekondari, vituo vya kutotolea wajasiriamali na makundi ya walemavu na wanawake.

Dk. Shein aliwaeleza wananchi na wageni waalikwa katika hafla hiyo iliyofanyika katika hoteli ya Zanzibar Beach Resort iliyopo nje kidogo ya Mji wa Zanzibar kuwa kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2009/2010 asilimia 17.1 ya vijana Zanzibar hawana ajira.

Kwa hiyo alieleza matumaini yake kuwa uzinduzi wa Mfuko huo utasaidia kwa kiasi kikubwa jitihada za Serikali za kuliwezesha kundi hilo pamoja na makundi mengine katika jamii kama la wanawake katika kuhakikisha kuwa kila mtu anatoa mchango wake katika ujenzi wa taifa.

"Hatuwezi kupata maendeleo ya kweli ikiwa tutakuwa na kundi kubwa la watu lililokuwa halizalishi kwa kukosa kushughulikiwa ipasavyo au kwa kukosa nyenzo za msingi za kuendesha maisha" Dk. Shein alieleza.

Alifafanua kuwa pamoja na jitihada za kuongeza fursa za mikopo lakini pia Serikali inaendeleza jitihada zake za kuhamasisha uwekezaji nchini hatua

ambayo itasaidia kuongeza ajira nchini. Alibainisha kuwa kuongezeka kwa fursa za elimu nchini kumepelekea kuwa na idadi kubwa ya vijana wanaomaliza masomo katika ngazi ya vyuo vikuu ikilinganishwa na nafasi za ajira zilizopo.

Kwa hiyo aliwahimiza vijana hao kuwa wabinifu na kuwa tayari kuanzisha vikundi vya ushirika katika fani walizosomea na kutolea mfano wa mafanikio waliyoyapata vijana wenzao huko India.

"...tunaweza kujifunza kutoka India ambako vijana wengi waliamua kuanzisha kampuni ndogondogo na vikundi vya ushirika katika tekinolojia ya habari na mawasiliano ambapo hivi sasa wamepata mafanikio makubwa baada ya kuibua masoko mapya hasa katika nchi za Ulaya na Marekani" Alifafanua Dk. Shein.

Alisisitiza kuwa Zanzibar inayo vijana mahiri wenye vipaji lakini akawataka kuondoa hofu ya kujaribu mambo mapya na kusema kuwa "hawataweza kuwa wajasiriamali wa kweli" kama watashindwa kuthubutu kufanya hivyo.

Katika mnasaba huo Mheshimiwa Rais alikumbushia umuhimu wa wananchi kuendeleza utamaduni wa kupenda vitu vinavyotengenezwa humu nchini kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia kuwaendeleza na kukuza masoko ya wajasiriamali nchini.

Pamoja na mambo mengine mfuko huo utakuwa na jukumu la kuanzisha ushirikiano na taasisi nyengine za fedha kama vile mabenki na kuwaunganisha wajasiriamali na taasisi nyengine kwa ajili ya kuwapatia mafunzo. Aidha mfuko huo utaweza kudhamini mikopo ya wajasiriamali inayotolewa kupitia taasisi mbali mbali za fedha.

Kwa upande mwengine wataalamu wa ujasiriamali na makundi mbali mbali wameemelezea matumainio yao kutokana na juhudi zinazochukuliwa na serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuleta maendeleo ya wananchi jambo ambalo limedhihirisha dhamira ya kweli ya serikali katika kukabiliana na umasikini.

Mtaalamu wa masuala ya ujasiriamali Dr. Rajeev Aggarwal amesema mwelekeo wa Zanzibar kuelekea kuondokana na umasikini ni mzuri, lakini amesisitiza haja ya kuwa na usimamizi mzuri wa mfuko huo ambao ameshauri kuweko na kamati maalum ya kusimamia mfuko itakayojumuisha wataalamu wa fani tofauti zinazohusiana na masuala ya biashara.

"Mahala pengine wajasiriamali hawahitaji fedha taslim "cash" wanaweza kutafutiwa vifaa (zana), mahala pengine utaalamu", alisema

Aidha, ameshauri kuwa Serikali hainabudi kuandaa utaratibu mzuri wa kuwasajili na kuwafuatilia kwa karibu wajasiriamali watakaonufaika na mfuko huo, siyo tu kwa kutaka kuhakikisha kuwa wanarejesha mkopo, lakini pia kuwasaidia kukabiliana na changamoto watakazokuwa wanakabiliana nazo katika hatua za mwanzo za biashara zao, kwani alisema tafiti zinaonesha kuwa idadi ya vifo vya makampuni ya biashara Zanzibar katika hatua za mwanzo ni kubwa.

Ndugu Haji Faraji Juma naye alikaririwa na jarida la Ikulu akisema kuwa, katika hatua ambayo Zanzibar imefikia hivi sasa, hakuna sababu ya mtu kulalamika kutokana na kuwa masikini mradi tu awe anapenda kujituma. "Kwa kweli hakuna sababu ya mtu kuilalamikia serikali; kama mikopo hii tutapewa, umeme upo, barabara safi zimejengwa hadi vijijini, huduma za elimu ya juu na vyuo vya amali zimeimarishwa, maji yanapatikana; tunataka nini tena?" alihoji Bwana Haji Faraji.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza wakati wa sherehe ya uzinduzi wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika ukumbi wa Zanzibar Beach Resort tarehe 21 Disemba, 2013.

Hali ya Uchumi
wa Zanzibar inaleta matumaini

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein

Misemo mingi ndani ya lugha ya Kiswahili hubeba maana nzito inapotafsiriwa katika mazingira halisi ya maisha ya mwanadamu ndani ya jamii anayoishi. Misemo kama vile "hakuna dhiki wa dhiki", "baada ya dhiki faraja" au "kimya kingi kina mshindo mkubwa", inakwenda sambamba na matukio na mwenendo wa maisha ya kijamii ya Wazanzibari, ambayo kwa muda mrefu yalikuwa yamegubikwa na mifarakano iliyotokana na uhasama wa kisiasa uliokuwa ukidumaza ukuaji wa uchumi na hivyo kukwamisha kasi ya maendeleo katika sekta zote.

Uhasama mkubwa wa kisiasa Zanzibar ulimalizika mwanzoni mwa mwezi Novemba mwaka 2010 baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kuteua viongozi wakuu wa Serikali; Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri wanaoongoza Wizara mbali mbali za Serikali, wakiwemo kutoka chama tawala cha CCM na Chama kikuu cha upinzani Zanzibar CUF.

Muundo au sura yenyewe ya Baraza la Mapinduzi inaonesha kumaliza tofauti za kisiasa Zanzibar ambazo tayari zilishaonesha ishara ya kuweza kuifikisha Zanzibar mahala pabaya. Kubwa zaidi linaloonesha kumalizika kwa mifarakano ya kisiasa iliyokuwa imedumu kwa karibu miaka 15 kabla ya kuundwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa kitaifa, ni namna viongozi wa pande hizo mbili (CCM na CUF) wanavyokaa pamoja kwenye Baraza la Mapinduzi kuzungumzia masuala muhimu yenye mustakbali wa Zanzibar.

"Huwezi kutofautisha vyama vyetu wakati tunapokaa na kujadiliana kuhusiana na masuala muhimu yenye maslahi ya nchi yetu na wananchi wetu wa Zanzibar, natamani sana siku moja nikualikeni katika mikutano yetu ya Baraza la Mapinduzi ili muone namna tunavyokaa pamoja bila ya kujali tofauti zetu za kisiasa katika kujadili mambo yenye maslahi ya nchi yetu, bahati mbaya sheria haniruhusu kufanya hivyo" alisema Dk. Shein alipokuwa akizungumza na wananchi wa Tumbe Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Hali ya maelewano miongoni mwa viongozi wa kisiasa imesababisha kuwepo kwa mazingira mazuri ya kukua uchumi nchini na kuzifanya sekta nyengine kukua vizuri ndani ya kipindi cha miaka mitatu tokea kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya saba yenye muundo wa Umoja wa kitaifa.

Wakati tunaadhimisha miaka mitatu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa, ni faraja na fahari kubwa kwa wananchi wa Zanzibar kuona kuwa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 - 2015 na mipango mikuu ya Serikali katika kukuza uchumi unakwenda kwa mujibu wa matarajio na mipango kama ilivyopangwa. Juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato, uwezeshaji, na ushirikishwaji wa wananchi katika harakati za kujenga uchumi zimekuwa zikizaa matunda mazuri.

Ukusanyaji wa mapato ya ndani umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2010/2011 Serikali ilikusanya Tsh. bilioni 181.4,

Sekta ya utalii imeonekana kukua kwa kasi katika siku za karibuni na kuchangia sehemu kubwa ya pato la Taifa nchini. Pichani ni wageni kutoka mataifa mbali mbali ya Ulaya ambao wamevutiwa na mazingira ya Zanzibar

mwaka 2011/2012, Tsh. bilioni 212 na katika mwaka 2012/2013 ukusanyaji ulikuwa Tsh. bilioni 266.2. Juhudi za kuimarisha Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) zinaendelezwa pamoja na kuimarisha mashirikiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Uchumi wa Zanzibar umekuwa ukikua kila mwaka. Ulikua kwa asilimia 6.4 katika mwaka 2010, ulifikia asilimia 6.7 katika mwaka 2011, asilimia 7.0 katika mwaka 2012 na unatarajiwa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2013.

Itakumbukwa kuwa wakati Serikali ya awamu ya saba inaingia madarakani, pato la Mtu Binafsi lilikuwa ni Tsh. 726,000 tu, na maelekezo ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, yalilenga Pato la Mtu Binafsi lifikie Tsh. 884,000 ifikapo mwaka 2015.

Jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na wananchi, zimefanikiwa kuliongeza Pato la Mtu Binafsi kutoka Tsh. 726,000 mwaka 2010 hadi kufikia Tsh. 960,000 mwaka 2011, ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani 611 kutoka Dola 560, mwaka 2010. Katika mwaka 2012, Pato la Mtu Binafsi liliongezeka na kufikia Tsh. 1,003,000 sawa na Dola za Kimarekani 638.

Huduma za benki zimeendelea kuimarishwa ili kutoa huduma nzuri kwa sekta binafsi ili nazo ziweze kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi na soko la ajira nchini. Mikopo ya Benki kwa sekta binafsi iliongezeka kutoka Tsh. bilioni 147.5 mwezi Septemba 2011 hadi kufikia Tsh. bilioni 150.9 mwezi wa Septemba 2012. Taasisi za kifedha zinaendelea kuimarika kutoka asilimia 4.0 mwaka 2011 hadi kufikia asilimia 10.2 mwaka 2012.

Licha ya mafanikio hayo tuliyoyapata hata hivyo, bado mfumko wa bei umekuwa ukileta changamoto kadhaa. Mwaka 2011 mfumko wa bei ulifika asilimia 14.7. Jitihada mbali mbali zimechukuliwa katika kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuimarisha shughuli za kilimo, kuwapunguzia wananchi ushuru katika baadhi ya bidhaa muhimu na kushajihisha uwekezaji. Mwaka 2012 mfumko wa bei ulishuka na kufikia asilimia 9.4. Hadi Disemba 2013 mfumko wa bei ulikuwa umefikia asilimia 5.0 kutoka asilimia 9.4 mwaka 2012.

Mafanikio ya katika ukuaji wa uchumi yanatokana na sababu nyingi lakini msingi mkuu ni kwa wananchi kuikubali serikali yao na kudumisha amani, utulivu na mshikamano mambo ambayo yamepelekea sekta nyingi kufanya vizuri katika kipindi kifupi cha miaka mitatu.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa Habari hivi karibuni, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, biashara ya usafirishaji na uingizaji wa bidhaa umeweza nao kuimarika, ambapo usafirishaji hasa wa karafuu umeongezeka hadi kufikia tani 2100 ambazo ziliozwa kwa Tsh. 11. 198 bilioni (USD 7.359.200) mwaka 2011, tani 4503 ambazo ziliozwa kwa Tsh. 84.184 bilioni (USD 58,057,660).

Uingizaji na utoaji wa bidhaa nchini umeweza kuimarika zaidi katika siku za karibuni. Pichani meli ya mizigo ikiteremsha bidhaa mbali mbali kwenye makontena kutoka nchi za nje.

mwaka 2012 - 2013 tani 2185 ambazo ziliuzwa kwa Tsh. 32.502 bilioni (USD 20, 617, 500). Bidhaa zenye thamani ya Tsh. milioni 271,273.1 ziliagizwa kutoka nje mwaka 2012 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamni ya Tsh. milioni 129,137 mwaka 2010.

Serikali imeweza kusimamia upandaji wa bei holela kwa bidhaa muhimu kama mchele, sukari na unga wa ngano kwa kuunda kanuni maalum za uagiziaji na kusimamia mwenendo wa biashara ambapo hivi sasa bei zinapangwa kwa mashirikiano ya pamoja baina ya serikali na wafanyabiashara wa ngazi zote.

Serikali imetoa ruhusa kwa wanaotaka kuagizia bidhaa hizo muhimu hapa Zanzibar, waagizie kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Wananchi wameombwa kuondokana na dhana kuwa kuna wafanyabiashara wachache ndio waliopewa vibali vya kuagizia bidhaa za namna hiyo. Jambo hilo sio kweli na wito unatolewa kwa wafanyabiashara wanaotaka kuagiza bidhaa toka nje wawasiliane na mamlaka husika ili waweze kupata vibali vya kufanya hivyo.

Tarehe 21 Agosti, 2011 Serikali imelifanyia mageuzi makubwa shirika la ZSTC na tayari imeshapitisha sheria mpya ya ZSTC yenye lengo la kuweka muundo mpya wa shirika hilo kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji, na kuweka majukumu mapya. Kwa upande wa biashara ya karafuu, Serikali inatekeleza mpango wa kuweka Utambulisho wa Karafuu ya Zanzibar (Branding) ili iweze kutambulika kimataifa na kupata hadhi na bei zaidi katika masoko ya dunia.

Katika kuimarisha mazingira ya biashara na viwanda nchini, Serikali imeamua kuifanya Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Kiuchumi (SEZ) ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imeanzishwa, ili kusimamia ubora na kuweka viwango vya bidhaa zinazozalishwa na zinazoingizwa nchini.

Jitihada za kuvifufua na kuvikuza viwanda hapa nchini zinaendelezwa, na katika kipindi cha 2011/12 jumla ya miradi tisa ya viwanda yenye jumla ya mitaji ya Dola za Kimarekani milioni 7.5 iliidhinishwa na Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA). Mchango wa sekta hii bado ni mdogo katika Pato la Taifa, hata hivyo ukuaji wake umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka.

Hivi karibuni ujenzi umeanza wa kiwanda kikubwa cha maziwa cha Azam Diary Factory katika eneo la Fumba, Unguja ambacho kitasarifu bidhaa za maziwa na kinatarajiwa kuajiri zaidi ya wafanyakazi 200. Aidha, kiwanda cha Sukari cha Mahonda kinaendelea kufufuliwa na wafanyakazi 350 wamepatiwa ajira.

Serikali imekuwa ikishajihisha ushiriki wa Sekta binafsi kuekeza katika viwanda kwa njia mbali mbali ikiwemo kupitia mikutano ya Baraza la Biashara la Zanzibar. Mafanikio hayo yanaashiria kufanikiwa vyema kwa serikali katika kutekeleza ilani ya CCM ifikapo mwaka 2015.

Yaoneni Maendeleo ya sekta ya Afya Zanzibar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia kuashiria ufunguzi wa Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya ikiwemo madarasa ya kusomea na Dakhalia kwenye majengo ya Chuo hicho yaliyoko Mbweni tarehe 7 Septemba, 2013

Kama ilivyo kwenye sekta nyengine za kijamii Zanzibar, imedhihirika kuwa licha ya kupata mafanikio makubwa tokea baada ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964, sekta ya afya imefanya vizuri katika kuimarisha huduma za afya kwa jamii ndani ya kipindi cha miaka mitatu tokea kuanza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliwaambia wananchi kupitia vyombo mbali mbali vya habari kwamba wanayo kila sababu ya kufurahia mafanikio makubwa yaliyoyapatikana katika Sekta ya hiyo ya afya.

Ukiacha mambo ya jumla ambayo yameendelea kutekelezwa tokea awamu zilizopita, kama vile ujenzi wa vituo 134 vya afya, ambavyo vimepelekea kupunguza masafa ya kutembea kupata huduma hadi kufikia chini ya wastani wa kilomita 5, huduma za afya zimeimarishwa pia kwenye hospitali 4 za koteji.

Kila hospitali moja kati ya hospitali hizo ina vitanda 40, na huduma muhimu zikiwemo za uchunguzi wa maradhi wa Maabara, huduma za meno, upasuaji mdogo na kadhalika vimeimarishwa. Kutokana na hatua hiyo, lengo la Serikali la kuziimarisha hospitali hizo ili ziweze kufikia kiwango cha hospitali za Wilaya, limefikia hatua nzuri; hasa kwa hospitali ya Koteji ya Makunduchi na Kivunge.

Pamoja na hatua hiyo, yapo mambo mengine ya msingi ambayo Serikali imeyafanya katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita katika kutekeleza Ilani ya CCM ya 2010 - 2015. Kwa mfano, katika kusimamia utekelezaji wa sera ya afya na ushirikishwaji wa wananchi na sekta binafsi katika kuchangia maendeleo ya afya kwa kuzingatia malengo ya Milenia, Dira ya 2020 na MKUZA, Serikali imezifanyia mapitio sera kadhaa pamoja na kushughulikia uanzishwaji wa bima ya afya.

Katika kuendelea kuimarisha huduma za Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili ifikie hadhi na kiwango cha Hospitali ya Rufaa, Serikali imeweza kufanya mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuweka Mtambo wa "Oxygen" kwenye chumba cha upasuaji (theatre), wodi ya wagonjwa mahututi (ICU), wodi ya wazazi (maternity) na chumba cha dharura na mashine ya kisasa ya kufanyia operesheni (minimal access surgery) kwenye chumba cha upasuaji.

Serikali imefungua "kituo cha meno cha tabasamu" (smiling center) kwa mashirikiano na wataalamu kutoka China na madaktari wazalendo wa Zanzibar kwa kufanya marekebisho kwa midomo yenye kasoro, Mfumo wa kuweka kumbukumbu za wagonjwa kwa kutumia kompyuta (Electronic medical Record System) umeanzishwa, vifaa vya kisasa vikiwemo kompyuta kwa ajili ya kazi hiyo vimewekwa sehemu ya mapokezi na umeanza kurikodi kumbukumbu za wagonjwa wa nje (OPD).

Mafunzo ya utafiti wa afya (clinical research) yametolewa kwa wafanyakazi 30 ili waweze kufanya tafiti mbali mbali na kusaidia kuimarisha huduma za afya, pamoja na kuifanyia ukarabati mdogo wodi ya wazazi na chumba cha wagonjwa wa dharura.

Mashirikiano na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland cha Norway yameendelezwa kwa kubadilishana wataalamu. Kwa mwaka 2013 wataalamu watano wa Zanzibar (madaktari wawili na wauguzi watatu 3) wamerejea kutoka Norway ambako walipata mafunzo kwa miezi sita wakati wafanyakazi watano (madaktari 2 na wauguzi 3) wa hospitali hiyo hivi sasa wapo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja wakisaidiana na madaktari na wauguzi wazalendo katika kutoa huduma bora za afya. Kurudi kwao kumeongeza ujuzi zaidi wa kukabiliana na kesi za maradhi mbali mbali.

Kadhalika, ipo miradi iliyobuniwa ambayo tayari imeanza kutekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa kuimarisha huduma za mama na mtoto, Mradi wa ujenzi wa jengo la wodi ya watoto, Mradi wa upasuaji wa maradhi ya kichwa na uti wa mgongo (Neurosurgical unit), Mradi wa kitengo cha "Gastro-Enterology", Mradi wa kuimarisha kitengo cha kisasa cha wodi ya wagonjwa mahututi (ICU) na Mradi wa elimu ya utafiti. Vile vile, maandalizi ya utibabu wa matatizo ya maradhi ya haja ndogo na figo yameanza.

Hospitali ya Wete imefanyiwa matengenezo katika wodi ya wanaume pamoja na vyoo vyake, kliniki ya watoto pamoja na kupatiwa vifaa vya kisasa. Aidha, imejengwa maabara mpya kubwa na ya kisasa kwa kushirikiana na "International Center for Aids care and treatment Programme" (ICAP) katika hospitali ya Micheweni.

Kwa kupitia mashirikiano yaliyoanzishwa baina ya hospitali ya Kivunge na mradi wa HIPZ, hospitali imefanikiwa kuanzisha kitengo cha huduma za dharura (Emergency Unit) kitakachotoa huduma za haraka kwa wagonjwa wanaofikishwa hospitalini hapo pamoja na kufanyiwa matengenezo kwa kituo cha elimu ya kujiendeleza (Resource Centre) iliyopo hospitalini hapo.

Katika kutekeleza mpango wa kuifanya Hospitali ya Abdalla Mzee kuwa hospitali ya Mkoa, mchakato umeanza ambapo Hospitali hii itajengwa kwa msaada mkubwa kutoka Jamhuri ya Watu wa China na itakuwa ni ya kisasa yenye uwezo wa kutoa huduma za wagonjwa wa maradhi mbali mbali na wagonjwa mahututi (ICU), huduma za dharura (accident and emergency) na huduma za uchunguzi wa "CT Scan".

Serikali iliahidi kukiimarisha Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya pamoja na watumishi wa sekta ya afya kwa kuwapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi. Utekelezaji wa ahadi hii umekwenda vizuri ambapo wafanyakazi 226 wamepelekwa mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi katika vyuo mbali mbali na Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya sasa kitaunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar SUZA katika kukiendeleza.

Katika kuziimarisha afya za wanawake, Serikali imeondoa ada ya Tsh. 40,000 kwa akinamama wanaokwenda kujifungua kwa operesheni. Kadhalika, huduma za bohari kuu ya dawa zimeimarishwa ili kurahisisha upatikanaji wa dawa nchini. Bohari Kuu mpya ya dawa ilifunguliwa rasmi huko Maruhubi katika shamrashamra ya Sherehe za Maadhimisho ya miaka 49 ya Mapinduzi mwezi Januari, 2013.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali imechukua juhudi maalum za kuiimarisha maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na sasa kwa mara ya kwanza imefanya uamuzi wa kumteua Mkemia Mkuu wa Serikali akiwa miongoni mwa wakurugenzi wa Wizara ya Afya. Maabara sasa itakuwa wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya na kuipatia ruzuku ambapo kwa mwaka wa fedha 2013/14 imetengewe Tsh. Milioni mia saba (shs. 700,000,000/=).

Mambo yanayoendelea kutekelezwa hivi sasa ni pamoja na kutayarisha mpangokazi wa miaka mitano, kutayarisha sheria ya kemikali, kanuni za wafanyakazi, mpango wa mafunzo ya ndani na nje na kufanya maandalizi ya ukarabati wa majengo mawili huko Maruhubi.

Mashine ya "CT Scan" iliyopo katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ambayo inachunguza matatizo mbali mbali ya afya ya binadamu.

Wanafunzi wa Chuo cha Taaluma ya Sayansi ya Afya Mbweni wakifanya majadiliano kuhusiana na masomo yao.

Sekta ya Elimu inavyozidi kuimarika

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia Vitabu vya aina mbali mbali kwenye Maktaba ya Skuli mpya ya sekondari ya Chasasa Pemba tarehe 23 Disemba 2013.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya saba inajivunia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya elimu kwa ujumla katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita ikitambua kuwa maendeleo ya nchi yoyote yanategemea kuwepo kwa fursa na elimu bora wanayoipata wananchi wake.

Mafanikio ya sekta hiyo yanatokana na jitihada kubwa za kuimarisha sekta ya elimu na yanaonekana wazi wazi katika elimu ya maandalizi, msingi, sekondari, utoaji wa elimu mbadala, mafunzo ya ualimu, elimu ya ufundi, mafunzo ya amali pamoja na fursa za elimu ya juu kwa wanafunzi wa Zanzibar.

Takwimu za Serikali katika masuala ya elimu zinaonesha kuwa Idadi ya skuli za Maandalizi zimeongezeka kutoka 238 zenye wanafunzi 1641 mwaka 2010 hadi skuli 278 zenye wanafunzi 30,912 mwaka 2013. Fursa ya Elimu ya msingi imeimarika kutoka skuli 299 zenye wanafunzi 226,746 mwaka 2010 hadi skuli 342 zenye wanafunzi 247,353. Wanafunzi walioandikishwa kuanza darasa la kwanza mwaka 2010 walikuwa 31,092. Mwaka huu wa 2013 watoto wote waliofikia umri wa kuanza skuli wameandikishwa idadi yao ikiwa ni watoto 35,703.
Hali hii imeifanya Zanzibar kupiga hatua kubwa ya utekelezaji wa malengo ya Milenia na yale ya Elimu kwa Wote. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa Sayansi na Teknolojia kwa watoto, Serikali imetekeleza Mradi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano uitwao T.21 kwa skuli za msingi 74 za Zanzibar.

Elimu ya sekondari imezidi kuimarishwa kwa kuongezeka kwa idadi ya skuli zinazotoa elimu hiyo kutoka kidato cha kwanza hadi cha sita, na hivi sasa zipo skuli za sekondari 252 zenye wanafunzi 84,099 kutoka skuli 227 zilizokuwa na wanafunzi 78,794 mwaka 2010. Serikali imekamilisha ujenzi wa skuli mpya za sekondari 13 kati ya 16 ambazo zimeshapatiwa samani na vifaa vya maabara na kuanza kutumika. Skuli 3 ambazo ni Paje - Mtule, Dimani na Tunguu ujenzi wake umefikia asilimia 94. Skuli hizi zilikuwa zikamilike mwaka 2015 kwa mujibu wa maelekezo ya Ilani na mipango ya awali, lakini Serikali imezikamilisha kabla ya wakati wake.

Katika uimarishaji wa elimu ya Sekondari, Serikali imekamilisha ujenzi wa skuli tatu za ghorofa katika maeneo ya Mpendae, Kwamtipura na Mazizini, zinazotarajiwa kufunguliwa katika sherehe za maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi. Aidha, ujenzi wa skuli nyengine mbili za ghorofa unaendelea vyema katika vijiji vya Kibuteni Mkoa wa Kusini Unguja na Mkanyageni katika Mkoa wa Kusini Pemba. Serikali vile vile, imekamilisha matengenezo makubwa katika skuli za sekondari za Forodhani na Tumekuja Unguja, na Utaani na Fidel Castro kwa Pemba. Matengenezo katika skuli za sekondari za Hamamni kwa Unguja na Uweleni Pemba yako katika hatua za mwisho kumalizika.

Aidha, kwa lengo la kuwaendeleza watoto wa kike katika masomo ya Sayansi, serikali imeamua kuzifanya skuli za sekondari ya Benbella Unguja na Utaani Pemba

zitumike kwa azma hiyo.

Fursa ya elimu ya juu nayo imezidi kuimarika kwa kuongeza idadi ya vijana wanaojiunga na elimu ya chuo kikuu hapa Zanzibar ambapo ndani ya kipindi hiki cha miaka mitatu vijana waliojiunga katika vyuo vikuu vya SUZA, Chuo cha Elimu Chukwani na Chuo Kikuu cha Zanzibar wameongezeka kutoka vijana 3,624 mwaka 2010 hadi vijana 4,485 mwaka 2013. Idadi hii haijumuishi vijana wanaoendelea kujisajli katika vyuo hivyo kwa mwaka wa masomo 2013 /2014.

Katika kipindi hiki Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kimeongeza idadi ya skuli za masomo kutoka skuli moja mwaka 2010 hadi skuli tano. Skuli hizo ni skuli ya Elimu Endelezi, skuli ya Elimu ya Lugha ya Kiswahili na Lugha za Kigeni na skuli ya Sayansi ya Asili na Jamii. Katika mwezi wa Oktoba, 2013 Skuli ya Tiba (Medical School) ilizinduliwa rasmi.

Vile vile, Chuo kimeanzisha shahada ya uzamifu (PhD) ya lugha ya Kiswahili. Sambamba na hatua hiyo, Chuo hiki kimeongeza idadi ya kampasi zake na kufikia tatu badala ya mbili ambapo sasa chuo kimepata haiba nzuri kwa kuanza kutumia kampasi yake mpya ya Tunguu iliyoanza kutumika mwaka 2012.

Kadhalika, ndani ya kipindi hiki Chuo Kikuu cha Zanzibar nacho kimeongeza masomo yanayofundishwa katika chuo hicho. Masomo yaliyoongezwa ni shahada ya Uzamili katika Utawala wa Umma na Sayansi ya Uchumi na Fedha. Masomo mengine ni ya Shahada ya Benki ya Kiislamu na Fedha, Shahada ya Teknolojia ya Habari na Uchumi, Shahada ya Lugha na Ualimu pamoja na Shahada ya Uuguzi. Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani nacho kimeimarisha masomo yake ikiwa ni pamoja na kuanza kusomeshwa kwa somo la lugha ya Kiswahili kwa wananchuo wa maandalizi (pre- university) na wa Shahada ya ualimu.

Ili kuwawezesha vijana wengi zaidi wanaopata sifa ya kuendelea na masomo yao vyuoni, Serikali imeongeza fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi kutoka Tsh. bilioni 2.3 mwaka 2010 hadi Tsh. bilioni 9.1 mwaka 2013. Serikali iliwapa mikopo waombaji wapya 1000 katika mwaka huu wa fedha wa 2013/2014. Serikali imechukua juhudi za makusudi ili kuongeza fedha kwa matumizi ya sekta ya elimu kwa ulinganisho wa matumizi ya serikali na Pato la Taifa kutoka asilimia 15.6 mwaka 2010 hadi asilimia 21.4 mwaka wa fedha uliomalizika wa 2012/2013.

Kadhalika, kwa upande wa madarasa ya kisomo kwa ajili ya wasiojua kusoma na kuandika, mafanikio yamepatikana kwa kupungua idadi ya watu wenye tatizo hilo na kuwa na wanakisomo 463 katika mwaka huu wa 2013 kutoka wanakisomo 6,980 mwaka 2010.

Sambamba na jitihada hizo, Serikali pia imeendelea kuimarisha mafunzo ya ualimu yanayotolewa katika chuo cha Kiislamu Mazizini, Chuo cha Kiislam Micheweni na Chuo cha Benjamin William Mkapa Kisiwani Pemba pamoja na mafunzo ya Ualimu na Daraja la 3A yanatolewa kwa utaratibu wa Elimu masafa kwenye vituo 9 vya walimu Unguja na Pemba. Katika mwezi wa Aprili, 2013 jumla ya walimu 675 walimaliza mafunzo yao ya cheti cha ualimu Daraja hilo.

Katika kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya amali, serikali imefanikiwa katika kuimarisha mazingira na taaluma inayotolewa katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia pamoja na vituo vya mafunzo ya amali vya Mwanakwerekwe na Mkokotoni kwa Unguja na Vitongoji huko Pemba.

Idadi ya wanafunzi katika taasisi ya Karume imeongezeka kutoka 237 mwaka 2010 hadi 1,215 mwaka 2012/2013. Kwa upande wa masomo ya kujiendeleza ya ufundi stadi, stashahada ya ICT, mafunzo ya Sayansi na Hisabati kwa elimu ya msingi na kidato cha nne, Taasisi ina jumla ya wanafunzi 996. Aidha, idadi ya wanafunzi wanaochukua masomo mbali mbali ya ufundi na amali katika vituo vya mafunzo vya Mwanakwereke, Mkokotoni na Vitongoji imeongezeka kutoka wanafunzi 449 mwaka 2010 hadi wanafunzi 784 mwaka 2012/2013.

Kwa jumla mafanikio ya sekta ya elimu yanaridhisha sana, licha ya changamoto zinazoikabili sekta hii ikiwemo uhaba wa walimu hasa wa sayansi, matokeo yasioridhisha ya mitihani ya Taifa, ukosefu wa samani na kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika baadhi ya madarasa ya skuli za mijini, uhaba wa fedha katika Bodi ya mikopo ya wanafunzi na nyenginezo.

Hata hivyo, mipango mizuri ya serikali na hali nzuri ya ukuaji wa uchumi inatia matumaini kuwa changamoto hizi zitaweza kutatuliwa hatua kwa hatua kwa ushirikiano na wananchi ikiwemo sekta binafsi kwa kuwekeza zaidi katika sekta ya huduma za jamii ikiwemo sekta ya elimu.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Sheina na Mkewe Mama Mwanamwema Shein pamoja na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Ali Juma Shamhuna wakipata maelezo kuhusu Maabara katika Skuli mpya ya sekondari ya Chasasa Pemba tarehe 23 Disemba 2013.

Tuwasaidieni

wanaoamua kuacha matumizi ya dawa za kulevya – Dk. Shein

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Bwana Abdulwahid Salum Said, Kiongozi wa Kituo cha Vijana walioamua kuacha Dawa za Kulevya (Sorber House) kilichopo Limbani, Wete, Pemba, wakati alipotembelea kituo hicho tarehe 19 Novemba, 2013.

Dawa za kulevya ni moja kati ya matatizo makubwa ya kiuchumi na kijamii hivi sasa ulimwenguni kutokana na athari wanazozipata watumiaji wa dawa hizo ambao wengi wao ni vijana. Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitembelea moja ya vituo vya vijana walioathirika na sasa wanapambana kuacha matumizi ya madawa hayo. Katika makala haya tunaelezea zaidi kuhusu ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kituo hicho.

Ziara ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kituo hicho ilifanyika ikiwa ni sehemu ya ratiba ya ziara yake ya siku tano kutembelea kisiwa cha Pemba kwa lengo la kukagua maendeleo ya msimu wa uchumaji karafuu pamoja na maendeleo ya ujenzi wa barabara katika mkoa wa Kaskazini Pemba. Limbani ni moja kati ya vijiji vilivyobahatika na mpango wa Serikali ya Awamu ya Pili ya ujenzi wa makaazi bora kwa wananchi maarufu nyumba za vijiji.

Kituo cha vijana walioamua kuachana na matumizi ya dawa za kulevya (Sobber House) cha Limbani hakiko mbali na mji wa Wete kiasi cha kilomita mbili kutoka katikati ya mji huo ukitokea Chakechake. Kipo upande wa pili wa barabara ukitokea Chakechake kikitazamana na nyumba za maendeleo.

Kama kawaida, ujio wa viongozi wakuu katika sehemu kama hii hutanguliwa na risala ya wenyeji kwa kuelezea shughuli husika inavyofanyika kwa kuainisha mafanikio, changamoto zilizopo na malengo ya baadae.

Risala ya vijana wa kituo pamoja na mambo mengine ilielezea historia ya kituo hicho na vituo vingine vilivyoko kisiwani Pemba. Ilibainisha kuwa kituo hicho ni kimoja kati ya vituo sita kama hivyo vilivyoko Pemba. Kati ya vituo hivyo vitatu viko mkoa wa Kaskazini na vingine vitatu viko Mkoa wa Kusini Pemba.

Risala ilieleza zaidi kuwa vituo vitatu vilivyoko Mkoa wa Kaskazini Pemba vimeanzishwa na kumilikiwa na kijana aitwaye Abdulwahid Salum Said ambaye mwanzoni alikuwa akiishi Mombasa nchini Kenya na kupatwa na masahiba ya kutumia dawa za kulevya lakini baadae aliweza kuacha na kurejea nyumbani ambapo aliamua kuanzisha vituo hivyo kusaidia wananchi wenzake.

Akizungumza na vijana hao, Mheshimiwa Rais aliwapongeza kwa uamuzi wao wa kijasiri wa kuachana na matumizi ya dawa za kulevya ambayo mbali ya kuwatia

umasikini na kuhatarisha afya zao, lakini pia matumizi ya dawa hizo huambatana na tabia au mwenendo ulio kinyume na maadili na kuathiri mahusiano yao na jamii.

Alimpongeza Bwana Abdulwahid kwa busara aliyoionesha pamoja na mapenzi kwa ndugu zake walioathirika na matumizi ya dawa hizo baada ya yeye mwenyewe kuwa alifikwa na mtihani huo na Mwenyezi Mungu akamjaalia kuushinda hadi kurejea nyumbani na kuanzisha vituo hivyo.

"Tunampongeza na kumshukuru ndugu yetu Abdulwahid ambaye mara baada ya kuzishinda dawa za kulevya huko nchini Kenya alikokuwa akiishi, aliamua kurejea nyumbani kusaidia ndugu zake walioathirika na dawa hizo" Dk. Shein alisema.

Alisema ni jambo la kushukuru kuona kuwa baada ya Abdulawahid kughafilika na kuingia katika matumzi ya dawa za kulevya, Mwenyezi Mungu amemuwezesha kujitambua na kurejea katika hali yake ya kawaida.

Dk. Shein alisema na kueleza kuwa ni bahati mbaya kuona baadhi ya wananchi wanawalaumu vijana wa aina hiyo badala ya kuwatia moyo na kuwapa kila msaada wanaouhitaji.

Alibainisha kuwa si jambo rahisi kwa watu wanaotumia dawa za kulevya kuacha na kurejea katika hali zao za kawaida hivyo jamii ni lazima iwaunge mkono vijana wanaoamua kuachana na matumizi ya dawa hizo.

Alieleza kuwa jamii inapaswa kuwapatia vijana hao kila msaada unaofaa ili kuhakikisha kuwa hawarejei tena kwenye matumizi ya dawa hizo ambapo kama ilivyoeleza risala yao wako baadhi wanaorejea katika matumizi ya dawa hizo kutokana na kukosa kuungwa mkono katika ngazi ya familia na hata jamii.

Kufuatia hali hiyo Mheshimiwa Rais alitoa wito wa kuwataka wazazi na kuitaka jamii kubadilika na kuwapokea tena kwa mikono miwili vijana waliofanikiwa kuacha matumizi ya dawa za kulevya.

Aliwakumbusha wazazi kuwa upotevu wa vijana hao haukati usuli wao na familia bali kama wahenga walivyosema "mtoto akinyea kiganja hakikatwi". Hivyo, vijana hao waliokosea hawana budi nao kukaribishwa tena katika jamii kwani bado ni watoto waliozaliwa na kulelewa katika jamii.

"wazazi hawana budi kukumbuka kuwa vijana hao ni watoto wao waliowazaa, kuwalea na kwamba pale mtoto anapopotoka na baadae kujirudi ni wajibu wao kuwapokea tena na kuwapa upendo kama zamani" alisisitiza Dk. Shein.

Kwa upande wa Serikali aliwahakikishia vijana hao kuwa itaendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha kuwa jitihada zao hazirejeshwi nyuma kwa sababu za unyanyapaa huo wa jamii dhidi yao na kukosa mahitaji ya msingi.

"Serikali ina kila sababu za kuwasaidia katika maisha yenu. Tunahitaji kuwalea, kuwaenzi na kuwapa huduma kama walivyo wananchi wengine" alibainisha Dk. Shein na kueleza kuwa Serikali ni mzazi. "Mzazi mzuri habagui, Serikali itafanya kila lililo ndani ya uwezo wake kwani ni jukumu letu kuendeleza jitihada zenu" alisema.

Kwa upande wake, uongozi wa kituo hicho ulieleza kuwa unafanya jitihada za kukabiliana na tatizo la jamii kuwakataa vijana hao kwa kuanzisha mpango wa kutoa ushauri nasaha kwa jamii kwa kuwatumia vijana walioacha madawa hayo ili kuivuta jamii kuona kuwa vijana hao bado ni sehemu ya jamii na ni rasilimali yenye mchango mkubwa kusaidia jamii yao.

Kiongozi wa kituo hicho Bwana Abdulwahidi Salim alieleza kuwa kazi wanayoifanya hapo ni ya kiroho kwa kuwarejesha vijana katika maisha yao ya kawaida na kuacha tabia ambazo zinaikera jamii ambazo ndizo zinazoifanya jamii kuwachukia na hata kukataa kuwapokea tena pale wanaporudi katika jamii.

"Tumekuwa tukifanya kazi ya kuwafanya vijana hawa sio tu kuacha dawa za kulevya, lakini pia kuacha tabia chafu zinazoichukiza jamii kama wizi, mauaji, ugomvi na uzinzi ambao unasababisha kusambaza virusi vya ukimwi" Alieleza Abdulwahid na kuvuta hisia za wananchi na viongozi waliokuwepo.

Katika mkutano huo Rais aliwaahidi vijana hao kuwa ataiagiza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuangalia namna bora ya kuimarisha huduma katika nyumba hizo Unguja na Pemba ili angalau ziweze kupata huduma nzuri zaidi japokuwa kwa kuanzia si kama walivyoomba katika risala yao.

"Hatuwezi kutoa majibu ya matatizo yenu yote hapa leo lakini kuhusu uimarishaji wa huduma hasa chakula katika nyumba hizi nitawasiliana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo ndio tuliyoikabidhi suala hili ili iweze kuzingatia maombi yenu hususan katika kupanga bajeti ya mwaka ujao wa fedha" aliahidi Dk. Shein.

Kuhusu suala la vijana hao kurudi katika jamii na kuendelea na maisha yao kama kawaida kwa maana ya ajira na shughuli nyingine za kujipatia riziki, Mheshimiwa Rais aliwasifu kwa kuwa na mipango mizuri ya kujiendeleza kielimu na kiajira. Alielezea kufurahishwa kwake na kutiwa moyo na namna vijana hao walivyojiwekea malengo ya kujiendeleza kielimu na pia kujishughulisha na miradi ya uzalishaji kama ufugaji na kilimo.

"Nimevutiwa na namna mlivyojidhatiti kukabiliana na changamoto zinazowakabili, sisi Serikali tunaahidi kujadiliana nanyi kuona namna mnavyoweza kushiriki katika ujenzi wa taifa" Dk. Shein aliwaeleza na kuwataka waainishe aina ya mafunzo wanayotaka ili Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iweze kuandaa utaratibu wa kuwapatia mafunzo hayo.

Kwa upande wa miradi aliwafahamisha kuwa Serikali inao mpango kabambe ambao nia yake ni kuwawezesha vijana kiuchumi ikiwemo kuanzisha miradi kama walivyoeleza katika risala yao.

"Tuna mpango wa kuzindua hivi karibuni Mfuko wa Uwezeshaji ambao lengo lake ni kuwasaidia wananchi wetu kujiajiri wenyewe katika sekta zote, nanyi tumieni fursa hiyo kwa kujiunga katika vikundi ili mfaidike na mpango huo" Dk. Shein aliwaambia vijana hao na kusisitiza kuwa lengo ni kuwajengea uwezo ili waweze kufanya wayatakayo kama ni ufugaji au kilimo.

Dk. Shein aliwaahidi vijana hao kuwa atawasiliana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuangalia namna ya kutekeleza ombi lao walilolitoa katika risala yao la kutaka wapewe fursa za kutoa elimu dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya maskulini.

Mbali ya maombi hayo, vijana hao waliomba kupatiwa kompyuta mbili ndogo (laptop) na magodoro 30, ambapo Mheshimiwa Rais alikubali na vifaa hivyo vilikabidhiwa siku iliyofuata na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ Mheshimiwa Haji Omar Kheri kwa niaba ya Mheshimiwa Rais.

Kwa hakika ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ilikuwa faraja kubwa kwa vijana hawa kwani iliwapa matumaini mapya na kujisikia ni sehemu ya jamii ambayo inastahiki heshma na upendo wa kila mwanajamii. Kitendo cha Mheshimiwa Rais kutimiza ahadi yake katika kipindi kifupi kilionesha dhamira ya kweli aliyonayo binafsi na Serikali anayoiongoza katika kuwasaidia vijana hawa.

Mafanikio ya Zanzibar

yanatokana na mshikamano, amani na utulivu – Dk. Shein

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisisitiza jambo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari Ikulu mjini Unguja tarehe 13 Novemba, 2013

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, tarehe 12 Novemba, 2013 alifanya mazungumzo na waandishi wa habari Ikulu mjini Zanzibar. Katika mazungumzo hayo alibainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu baada ya kuingia madarakani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa anayoiongoza.

Amesema kwa kiasi kikubwa mafanikio hayo yamepatikana kwa mashirikiano makubwa walioyaonesha wananchi wa Zanzibar, ambapo amani, utulivu na mshikamano imeonekana kuwa ndiyo chachu ya mafanikio hayo kuelekea kufikia kwenye malengo ya jumla ya Serikali. Alitoa wito kwa wananchi wa Zanzibar kuendelea kushirikiana na Serikali ili iweze kufikia malengo yake. Ifuatayo ni sehemu ya hotuba ya Rais wa Zanzibar kwa wananchi.

…..Napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa wananchi wote kwa kushirikiana na Serikali. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wataendelea kushirikiana na Serikali na vile vile wafanyakazi wote wa Serikali wataendelea kuongeza juhudi zao ili tuweze kutekeleza malengo yetu ya DIRA YA MAENDELEO 2020. Hivi sasa tumebakiwa na miaka sita tu hadi kuyafikia malengo hayo. Pindi kama tukiyafikia, hapana shaka tutaitoa nchi katika kundi la nchi za kipato cha chini na kuwa katika kundi la nchi za kipato cha kati (Middle income).

Bila ya shaka yoyote, hali hiyo tutaifikia tu tukiwa makini, watiifu wa amani na utulivu nchini. Utiifu wa sheria ni hatua moja muhimu katika kuyafanikisha hayo. Ni jukumu la viongozi wote wa Serikali, wanasiasa, viongozi wa dini na viongozi wengine katika jamii, sote kwa pamoja tutekeleza wajibu wetu kwa kuhakikisha kwamba amani na utulivu unadumishwa na sheria za nchi zinafuatwa.

Ilivyokuwa Serikali inaongozwa kwa misingi ya Katiba na Sheria zake, basi vyama vyote vya siasa, taasisi zisizokuwa za Serikali na zile za jamii nazo ni lazima ziongozwe kwa kuzingatia katiba za nchi, katiba zao, kanuni zao na kuzifuata sheria za nchi. Sura ya Tatu ya Katiba yetu imeelezea kuhusu Kinga ya Haki za Lazima, Wajibu wa Uhuru wa Mtu Binafsi, kuanzia kifungu cha 11 hadi kifungu cha 25.

Lakini kila mtu ana wajibu wa kufuata na kuitii Katiba ya Zanzibar na Sheria zake. Hili ni jambo muhimu. Lazima tuyaenzi na tuyadumishe Mapinduzi yetu na tuudumishe na tuuendeleze Muungano wetu kwani ndiyo nguzo yetu kubwa ya maendeleo na vilivyotufikisha hapa tulipofika hivi sasa na tunakokusudia kufika katika miaka mingi ijayo.

Katika kipindi hiki tumeshuhudia Muungano wetu umeendelea kuwa imara zaidi tangu pale ulipoanzishwa na nchi yetu imepata heshima kubwa sana katika Jumuiya ya Kimataifa. Tumepata mafanikio makubwa ya kisiasa, kiuchumi na ustawi wa jamii, ingawa zimekuwepo baadhi ya changamoto lakini zitaendelea kushughulikiwa hatua kwa hatua.

Napenda niwahakikishie wananchi wote kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza Muungano wetu, kuimarisha na kuwatumikia wananchi. Katika kuuimarisha Muungano wetu, sote tumetimiza wajibu kwa kutoa maoni yetu kwa ajili ya kuandaliwa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba Mpya imefanya kazi nzuri na itaendelea kuifanya kazi hiyo kama vile sheria inavyoiongoza. Hatua zilizobakia nazo zitakamilishwa kwa kuzingatia sheria iliyopo ili hatimae tupate Katiba Mpya itakayoliongoza Taifa letu na kuimarisha Muungano wetu.

Napenda nimshukuru na nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kusimama imara katika kuutetea na

Waandishi pamoja na Wahariri wa vyombo mbali mbali vya habari wakimsikiliza kwa makini Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza nao Ikulu mjini Unguja tarehe 13 Novemba, 2013

kuuendeleza Muungano wetu na kwamba siku zote yuko tayari kuzizungumzia changamoto zinazoukabili Muungano wetu na kutafuta njia za kuzipatia ufumbuzi kila zinapotokea.

Hivi sasa tumemaliza miaka mitatu tangu SMZ yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa imeingia madarakani. Hata hivyo, bado ipo kazi kubwa mbele yetu ambayo inahitaji jitihada zetu sote. Tuendelee kushikamana na kupendana, tushindane kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa bila ya kugombana, bila ya kukashifiana, bila ya kulaumiana, bila ya kutukanana na bila ya kudharauliana. Zanzibar hata siku moja haitajengwa kwa mambo hayo yasiyokuwa na tija wala faida. Huu ni wakati wa kuongeza kasi na kuijenga nchi yetu, ili tusije tukaachwa nyuma.

Napenda kuwahakikishia wananchi wote wa Zanzibar kuwa Serikali kwa upande wake itaendelea kutekeleza wajibu wa kikatiba na sheria kwa kuilinda amani, utulivu, mali na maisha ya watu. Hakuna atakayedhulumiwa wala kuonewa, lakini pia hakuna atakayevumiliwa kwa kuvunja sheria.

Tukiwa tumo katika kipindi cha shamrashamra ya kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, natoa wito kwa kila mmoja wetu awe ni sehemu ya kuzifanikisha sherehe zetu kwa furaha, salama, amani na utulivu. Tushirikiane sote kwa pamoja na tuendeleze umoja na mshikamano katika kuzifanikisha sherehe zetu, ili tuioneshe dunia mafanikio yetu ya miaka 50, utamaduni wetu na kwamba tunauthamini umoja wetu, amani na mshikamano wetu.

Muungano umeimarisha undugu na umoja wa Watanzania

Suala la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar limekuwa agenda kubwa miongoni mwa Watanzania ambao miongoni mwao wanafahamu kwa undani faida, hasara, mafanikio na changamoto zake. Lakini wapo miongoni mwa watanzania ambao hawana uelewa wa kutosha kuhusiana na masuala ya Muungano na wamekuwa wakishabikia kile kinachoelezwa na wenye vipaji na utashi vikinasibishwa na mitazamo binafsi kuhusiana na suala hilo.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika mikutano yake tofauti na wananchi wa Zanzibar amekuwa akisisitiza umuhimu wa kuudumisha Muungano kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Katika makala hii tunajaribu kuelezea angalau kwa ufupi masuala machache yanayohusiana na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao umedumu kwa takriban miaka 50 sasa.

Mara nyingi mafanikio yoyote huenda sambamba na changamoto. Ili ufanikiwe unalazimika kukabiliana na changamoto za aina mbali mbali. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo karibuni inatimiza miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar haitafautiani na nchi nyengine katika kufikia maendeleo endelevu. Ingawa zipo baadhi ya changamoto, lakini mafanikio makubwa yamepatikana.

Muundo wa Muungano wenyewe ni wakipekee na haujafanyika katika nchi yoyote ya Afrika. Chini ya mfumo huu wa

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akibadilishana mawazo na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dk. Mohamed Gharib Bilal wakati wa tafrija iliyofanyika kwenye viwanja vya Ikulu ya Mjini Dar es Salaam tarehe 09 Disemba, 2013. Kulia ni Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein, na kushoto ni Mke wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Asha Bilal.

Muungano, Tanzania imeweza kuimarisha ulinzi na usalama ndani ya mipaka yake dhidi ya maadui wa ndani na nje ya nchi. Kwa Zanzibar, Muungano huu ndio ngao imara ya kuyalinda Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964.

Muungano huu umeimarisha kujenga undugu, umoja na mshikamano baina ya wananchi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ulikuwa wa enzi na enzi. Historia inatufundisha kuwa watu wote wanaoishi katika visiwa ni wahamiaji kutoka katika maeneo mbali mbali. Hii inatuthibitishia kuwa Wazanzibari wote ndani ya visiwa hivi wamehamia kutoka maeneo tofauti. Kinachowatafautisha ni nani alifika mwanzo na nani alifika baadae. Hivyo, Muungano huu umeimarisha undugu kwa watu kuishi pamoja.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka uhuru kwa watu wa pande hizi mbili kwenda kokote wanakotaka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuishi na kufanya kazi bila ya kubugudhiwa. Hii ni faida kubwa kwa Watanzania na hasa kwa Wazanzibari ambao wanaruhusiwa kuishi sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na fursa hii, wananchi wengi wa Zanzibar wameweza kuhamia mikoa mbali mbali ya Tanzania

Viongozi wa Kitaifa wakiwa katika sherehe za Uhuru wa Tanganyika zilizofanyika katika kiwanja cha Uhuru Mjini Dar es Salaam akiwemo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tarehe 09 Disemba, 2013.

Bara wakiendesha shughuli mbali mbali za maisha kwa uhuru kabisa na mafanikio makubwa.

Kama ilivyoelezwa awali, kwenye mafanikio hapakosi changamoto. Ndani ya Muungano wa huu zipo baadhi ya changamoto ambazo baadhi ya watu wamekuwa wakizichanganya changamoto za Muungano na kero za Muungano. Serikali ya Jamhuri ya Muungano imefikia hatua nzuri katika kuzitafutia ufumbuzi kero nyingi za Muungano kupitia vikao vya pamoja vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa mfano;

Suala la ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki limekuwa likizungumzwa kuwa ni kero. Lakini Wizara ya Afrika Mashariki pamoja na sekretarieti yake inaendelea na jitihada za kutafuta ufadhili wa miradi ya Zanzibar iliyowasilishwa kwenye sekretarieti hiyo. Juhudi hizo zilikuwa zimekwama kutokana na kuchelewa kidogo kufanyika upembuzi yakinifu wa mradi wa uwanja wa ndege wa Pemba na kufanyika kwa mchanganuo wa mradi wa ujenzi wa bandari ya Maruhubi. Mradi wa ujenzi wa chelezo na kivuko katika bandari ya Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Tanga na Mombasa bado ni kipaumbele ingawa bado inafikiriwa. Hatua nzuri imefikiwa kuhusiana na suala hili.

Kamati ya wanasheria wakuu wa SMT na SMZ na wataalamu wa sekta ya nishati wa pande hizo mbili imeshaundwa kama ambavyo iliagizwa na tayari imeshaandaa hadidu za rejea kuwezesha kutekeleza maagizo ya kamati ya pamoja ya SMT na SMZ ambayo imeshakutana mara kadhaa kuzungumzia suala la utafutaji wa mafuta na gesi asili, ambalo nalo linatajwa kuwa ni miongoni mwa kero za Muungano. Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali ilishauriwa kuiandikia barua SMZ ili kuiruhusu SMZ kuendelea na matayarisho ya utafutaji wa mafuta na gesi asili. Utekelezaji tayari umeanza.

Suala la Uvuvi kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu nalo limeelezwa kuwa ni kero ya Muungano. Kimsingi imeshakubalika kwamba SMZ inaweza kutumia njia mbadala ya kumaliza suala hili kwa kupeleka sheria ya mamlaka ya uvuvi kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu kwenye Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuorodheshwa na mchakato unaendelea.

Rasimu ya muongozo wa ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yote ya kikanda na kimataifa umeshawasilishwa, kujadiliwa na kuridhiwa. Hatua hii inalenga katika kuimarisha ushirikiano wa moja kwa moja wa Zanzibar na nchi za nje jambo ambalo nalo lilikuwa miongoni mwa zile zinazoelezwa kuwa kero za Muungano.

Kuhusu ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika taasisi za Muungano, mwongozo wa utekelezaji kuhusu utaratibu wa muda wa mgao wa ajira katika taasisi za Muungano umekamilika na umeshasambazwa kwenye Wizara husika.

Wizara zinazoshughulikia masuala ya Fedha za SMT na SMZ zimeshakutana na kukubaliana kuwa hati ya makubaliano baina ya SMT na washirika wa Maendeleo ifanyiwe marekebisho ili MKUZA iingizwe kwenye hati hiyo kama ilivyofanyika kwa MKUKUTA. Aidha, ilishakubaliwa kwamba washirika wa maendeleo wajulishwe kuhusiana na suala hilo. Hatua hii inalenga katika kulitafutia ufumbuzi suala la mgawanyo wa Mapato yatokanayo na misaada kutoka nje ya nchi ambalo nalo lilikuwemo kwenye orodha ya kero za Muungano.

Mawaziri wa Fedha wa SMT na SMZ wameshakutana mara kadhaa kujadiliana kuhusiana na Malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili na wamekubaliana kuwa, TRA ifanye mapitio ya mfumo mpya wa kufanya tathmini kwa lengo la kubaini faida na upungufu wake na baadae kuwasilisha taarifa kwa mawaziri wa pande zote mbili ili iweze kufanyiwa kazi. Mchakato huo umefikia hatua nzuri.

Kimsingi masuala yote ambayo yameonekana kuwa ni kero au changamoto katika Muungano, yanaweza kushughulikiwa katika vikao vya pamoja vinavyoendelea, na kwamba hakuna lisilowezekana mradi tu busara zinahitajika katika kila eneo.

Suala kuhusu muundo au mfumo wa Muungano limepata mjadala mkubwa kuliko masuala mengine yote ambayo yangepaswa pia kuzungumzwa kwenye mapendekezo ya katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni fursa ya kikatiba ambayo imetolewa kwa wananchi na ni haki ya kila mtu kutoa maoni yake kama atakavyoona inafaa.

Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla hawana budi kuulinda Muungano kwa maslahi yao ya sasa na vizazi vijavyo kwani muungano ndio ngao ya mapinduzi.

Zanzibar
yahuzunika na kifo cha Nelson Rolihlahla Mandela

Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa awamu ya nne Mzee Idrissa Abdulwakil akiwa na mgeni wake aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini Nelson Mandela alipofika Zanzibar tarehe 7 Machi, 1990, kushoto ni Dk.Omar Ali Juma aliyekuwa Waziri Kuongozi wa Zanzibar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na wananchi wa Zanzibar wameungana na viongozi na wananchi ulimwenguni kote kuomboleza kifo cha Rais wa zamani wa Afrika Kusini Nelson Rolihlahla Mandela kilichotokea tarehe 5 Disemba, 2013 na kuzikwa tarehe 15 Disemba, 2013.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimtumia salamu za Rambirambi Rais wa Afrika Kusini Bwana Jacob Zuma kufuatia kifo hicho cha Mzee Nelson Mandela ambaye ni Rais wa Kwanza Mwafrika kuiongoza nchi hiyo tangu kutokomezwa kwa siasa za ubaguzi wa rangi nchini humo.

Katika salamu hizo Dk. Shein amesema yeye binafsi na wananchi wote wa Zanzibar wamepokea kwa masikitiko na huzuni kubwa taarifa za kifo cha Bwana Mandela.

Amesema maneno pekee hayawezi kueleza huzuni, hisia na jinsi wananchi wa Zanzibar walivyoguswa na kifo cha Mzee Mandela na amewahakikishia wananchi wa Afrika Kusini kuwa wananchi wa Zanzibar wako pamoja nao wakati wakiomboleza msiba huo mkubwa.

"Mandela alikuwa na ataendelea kuwa kielelezo cha uhuru na haki ulimwenguni. Kwetu sisi Afrika ataendelea kuwa alama ya ukombozi. Alionesha mwangaza pale palipokuwa na kiza, na ilikuwa ni mwangaza wake uliong' arisha ulimwengu kwa utu." ameeleza Dk. Shein na kuongeza kuwa dunia itaukosa mwangaza huo.

Dk. Shein amemuelezea pia Bwana Mandela kama mtetezi mkubwa na kiongozi aliyepigania utu wa mwanadamu na kwamba alitumikia maisha yake katika ukombozi na kutetea haki hivyo dunia daima itakuwa na deni kwake.

"Nakutumia salamu za rambirambi wewe binafsi Mheshimiwa Rais, kwa kuwa umekuwa mmoja wa watu wa karibu sana na ndugu Madiba" alisema Dk. Shein katika salamu zake hizo kwa Rais Zuma.

Kupitia kwa Rais wa Afrika Kusini Jacob Zuma, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameipa pole familia ya Marehemu Nelson Mandela, jamaa na wananchi wa Afrika Kusini.

Makamu wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi akifuatana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete alitoa salamu za pole kutoka kwa wananchi wa Zanzibar kwa viongozi na wananchi wa Afrika Kusini.

Mzee Nelson Mandela aliongoza harakati za watu weusi dhidi ya utawala wa kibaguzi wa rangi nchini humo na katika harakati hizo alipata msaada mkubwa kutoka kwa viongozi na wananchi wa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania.

Mara baada ya kutolewa gerezani mwezi Machi, 1990, Mzee Mandela alifanya ziara rasmi kuzitembelea nchi mbalimbali zilizokuwa zikiunga mkono harakati za wananchi wa Afrika Kusini dhidi ya ubaguzi wa rangi nchini mwao. Ziara hiyo ilimfikisha nchini Tanzania kuwashukuru viongozi na wananchi wa Tanzania kwa mchango wao uliomuwezesha yeye kufunguliwa gerezani.

Akiwa nchini Tanzania tarehe 7 Machi, 1990, Mzee Mandela alifika Zanzibar kwa ziara ya siku moja ambapo alikutana na viongozi na kuhutubia maelfu ya wananchi waliokuwa wamefurika katika uwanja wa Amaan. Kama ilivyoripotiwa katika vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi siku hiyo mji wa Zanzibar ulifurika. Wananchi wakiwa na shauku ya kumuona Mzee Mandela walijaa kwenye barabara inayotoka uwanja wa ndege wa Zanzibar ambako alipokelewa na uwanja wa Amani ambako alihutubia wananchi.

Katika hotuba yake aliyoitoa uwanja wa Amaan, Mzee Mandela aliwaeleza wananchi namna alivyomfahamu Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Mzee Abeid Amani Karume na mazungumzo yao waliyofanya mjini Adis Ababa Ethiopia walipokutana huko mwaka 1962. Mzee Mandela aliomba apelekwe alipozikwa Mzee Karume na alipopelekwa Ofisi Kuu ya CCM alipata fursa kuona sehemu aliyouawa Marehemu Mzee Karume.

MATUKIO MBALI M

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein alipokuwa akiangalia maonesho ya wajasiriamali wakati wa uzinduzi wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika ukumbi wa Zanzibar Beach Resort nje ya Mji wa Unguja tarehe 21 Disemba, 2013

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kuashiria ufunguzi wa kituo cha Afya cha Kijiji cha Kajengwa Makunduchi Wilaya ya Kusini Unguja, katika shamra shamra za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 16 Disemba, 2013.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia maonesho ya kazi mbali mbali wakati wa uzinduzi wa Komngamano la Utafiti na Ubunifu lililofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Zanzibar Beach Resort tarehe 19 Disemba, 2013.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na watendaji, maafisa wadhamini, maafisa tawala na Wakuu wa Mikoa Mikoa ya Pemba alipokuwa katika ziara maalum kisiwani humo tarehe 23 Novemba, 2013.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akibadilishana mawazo na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Ali Juma Shamhuna katika sherehe za ufunguzi wa skuli ya sekondari ya wanawake ya Utaani na Skuli ya sekondari ya Chasasa tarehe 23 Disemba, 2013

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Mwakilishi UN wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya Ukimwi Duniani katika Kijiji cha Paje Wilaya ya Kusini Unguja tarehe 01 Disemba, 2013.

BALI KATIKA PICHA



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiagana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete baada ya dhifa ya chakula cha Mchana Ikulu Jijini Dar es Salaam siku ya Uhuru wa Tanganyika tarehe 09 Disemba, 2013

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Mohamed Gharib Bilal wakiwa na wake zao katika sherehe za maadhimisho ya siku ya Uhuru wa Tanganyika katika viwanja vya Ikulu mjini Dar es Salaam tarehe 09 Disemba, 2013

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akizungumza na wanaushirika wa vikundi mbali mbali kwa vya Mkoa wa Kaskazini Pemba wakati wa ziara yake Wilayani humo tarehe 18 Disemba, 2013

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na wananchi katika maadhimisho ya siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Kijiji cha Paje Wilaya ya Kusini Unguja tarehe 01 Disemba, 2013

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein na Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mama Asha Balozi wakiangalia bidhaa mbali mbali zilizotengenezwa na wajasiriamali wa Pemba tarehe 18 Disemba, 2013

Wake wa Viongozi wa Kitaifa na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa mataifa Dk. Asha Rose Migiro wakiwa katika picha ya pamoja siku ya kilele cha Uhuru wa Tanganyika baada ya dhifa ya chakula cha mchana iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 09 Disemba, 2013

Ziara ya Mama Mwanam

Kama kulikuwa na tatizo kubwa ambalo kwa muda mrefu lilikuwa likiisumbua Zanzibar, Afrika na duniani kote, basi lilikuwa ni suala la akinamama kuanchwa nyuma katika hatua zote za kimaendeleo kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Kilio cha akinamama kilienea ulimwenguni kote hadi ulipofanyika mkutano mkuu wa nne wa wanawake mjini Beijing China mwezi Septemba 1995, ambapo wanawake duniani wenyewe walifikia maazimio kadhaa yenye lengo la kuilinda hadhi na heshima yao sambamba na kupiga vita aina zote za ubaguzi wa kijinsia.

Katika maazimio yao, wanawake wametaka kushirikishwa kikamilifu katika masuala yote ya kupanga, kuamua na kutekeleza masuala yote ya kitaifa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, uhifadhi wa mazingira na yote yanayohusiana nayo bila ya kujali maumbile yao kijinsia.

Ni dhahiri kwamba serikali nyingi duniani zimeamua kubadilika mara tu baada ya kumalizika kwa mkutano huo, na Zanzibar ambayp ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya mataifa ya kupigiwa mfano katika kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa fursa sawa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Idadi ya wanawake kwenye mabaraza ya kutunga sheria – Bunge na Baraza la wawakilishi imekuwa ikiongezeka kwa kiasi cha kuridhisha. Aidha, uteuzi wa nafasi mbali mbali unaofanywa wa viongozi wakuu wa serikali umekuwa ukizingatia kwa makini masuala ya kijinsia. Sera za kitaifa nazo zimekuwa zikiweka msisitizo maalum masuala ya kijinsia pamoja na makundi yote yaliyomo ndani ya jamii.

Lakini sehemu kubwa katika kufanikisha azma ya kumkomboa mwanamke imekuwa ikifanywa na wanawake wenyewe wakiwemo wake wa Marais. Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mama Mwanamwema Shein siku zote amekuwa mstari wa mbele kuwashajiisha akinamama kuchangamkia fursa zilizopo ili kuondokana na umasikini.

Akizungumza na akinamama wa Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba Pemba hivi karibuni Mama Mwanamwema Shein amesisitiza haja ya akinamama kuzitumia fursa zilizopo ndani na nje ya serikali kupitia miradi mbali mbali ya maendeleo vikiwemo vikundi vya uzalishaji ili kuweza kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umasikini.

Changamkieni fursa zilizopo muondokane na umasikini

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akizungumza na wanaushirika wa vikundi mbali mbali kwa vya Mkoa wa Kaskazini Pemba wakati wa ziara yake Wilayani humo tarehe 18 Disemba, 2013

Wito huo wa Mama Mwanamwema Shein unatokana na ukweli kwamba akinamama wanao mchango mkubwa na muhimu katika maendeleo ya taifa hivyo ni vyema kuzitumia fursa zilizopo za kuwapatia maendeleo na kuongeza mchango wa kasi ya maendeleo kwa taifa na familia zao.

Alitoa wito wakati aplipokuwa akizungumza na akinamama wa mikoa miwili ya Kaskazini na Kusini Pemba katika mikutano tofauti aliyoifanya katika ukumbi wa Jamhuri hall Wete na ukumbi wa skuli ya Fidel Castro Chake chake Pemba mara baada ya kuvitembelea vikundi vya uzalishaji wa kilimo, mifugo na upandaji wa miti katika ziara yake iliyofanyika kisiwani Pemba hivi karibuni.

Ziara ya mke wa rais wa Zanzibar mama Mwanamwema Shein kwenye vikundi hivyo imefanyika wakati wananchi wa Zanzibar wakisherehekea kutimia miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964. Akinamama wanayo kila sababu ya kukumbuka mchango wa akinamama wenzao waliojitolea katika harakati za siasa zilizosaidia kuleta uhuru wa wananchi katika visiwa vya Unguja na Pemba chini ya chama cha ASP.

Mama Mwanamwema Shein amewataka akinamama kushajiishana katika kuanzisha vikundi vya ushirika, ujasiliamali na SACCOS ikiwa ni njia mojawapo ya kuongeza mitaji yao ya uzalishaji.

Akizungumzia juu ya wajibu wa akinamama katika kuwalea watoto wao mama Shein amewakumbusha akinamama hao kurejesha malezi bora kwa watoto wao na kuwapa miongozo mizuri itakayowafaa kwa maisha yao ya baadae na kuwaepusha na majanga yakiwemo ya madawa ya kulevya na ukimwi.

nwema Kisiwani Pemba

Katika ziara yake hiyo mama Mwanamwema Shein ambaye alifuatana na mama Asha Suleiman Iddi, Mke wa Balozi wa China mama Wu Yan walikabidhi vifaa mbali mbali kwa vikundi vya akinamama vikiwemo cherehani, nyuzi na vifaa vyengine vya kuendeshea shughuli za vikundi mbali mbali vya uzalishaji.

Vikundi vilivyofaidika na misaada hiyo kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba ni kikundi cha ushirika cha Tupendane chenye wanachama 15 wanaojishughulisha na shughuli za ushoni wa nguo za kike na ufumaji wa mashuka, kikundi cha Allah Atosha chenye wanachama 21 wanaojishughulisha na kilimo cha migomba, ufumaji na saloon na kikundi cha Nia Njema kinachojishughulisha na utengenezaji wa nguo za batiki. Kikundi kingine ni Tuhasike chenye wanachama 21 wanaojishughulisha na ufugaji wa ng' ombe wa maziwa na kazi za ufinyanzi wa vyungu na mikungu.

Kwa upande wa Mkoa wa Kusini vikundi vilivyofaidika na misaada hiyo ni kikundi cha Nia Safi SACCOS shughuli zao za ufugaji na ushoni, Hatugombani wanajishughulisha na upandaji wa miti ya mivinje na mikaratusi, Mkarafuuni Cooperetive Sociaty shughuli za uzalishaji mali na ushirika wa Wambaa ambao wanajishughulisha na kilimo na shughuli nyengine za uzalisjai.

Katika risala zao walizotoa kwa viongozi hao wameomba kutafutiwa masoko ya kuuzia bidhaaa zao kwani pamoja na juhudi kubwa wanazozichukua za uzalishaji, bado hawana masoko ya uhakika ya kuuzia bidhaa zao jambo ambalo walisema linarejesha kasi ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa zao.

Hata hivyo wamempongeza mama Mwanamwema Shein na mama Balozi Seif Ali Iddi kutokana na juhudi kubwa ambazo wamekuwa wakizichukua katika kuwahamasisha akianama kujiendeleza kiuchumi na kuondokana na hali ya umasikini.

Wamesema ziara zinazofanywa na wake hao wa viongozi zimekuwa zikileta nguvu kwa akinamama wengine na kuthamini misaada yao na wamewahakikishia kuwa wataitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili hatimaye waweze kuongeza uzalishaji wa bidhaa zao jambo ambalo pia litaimarisha vikundi vyao.

Wakati huo huo Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein amepokea hundi ya shilingi milioni tano kutoka kampuni ya "Sinohydro Tiajing Enginearing Co. Ltd ya China kwa ali ya kusaidia miradi ya jamii kupitia Umoja wa Wake wa Viongozi wakiwemo wake wa wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakiklishi kutoka Chama Cha Mapinduzi.

Akipokea hundi hiyo kutoka kwa Bwana Wang Jingli, Mama Mwanamwema Shein ameipongeza kampuni hiyo kutokana na msaada huo ambao amesema utawanufaisha wanawake wote wa Unguja na Pemba.

"Tunakuhakikishia kwamba misaada ya aina hii itawafikia walengwa hasa wa vijijini bila ya kujali itikadi zao za kisiasa" alisema Mama Shein.

Akinamama wa mikoa miwili ya Pemba wamepongeza na kusifu ziara zinazofanywa na Mama Mwanamwema Shein, Mama Asha Balozi Iddi pamoja na baadhi ya wake wa viongozi wa wabunge na wawakilishi na wametoa wito kwa wengine kuiga mfano huo kwani wamesema ziara za aina hiyo zinaongeza kasi na ari ya akinamama kujituma zaidi na kuongeza kasi ya uzalishaji kupitia vikundi vyao vya ushirika.

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein na Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mama Asha Balozi wakiangalia bidhaa mbali mbali zilizotengenezwa na wajasiriamali wa Pemba tarehe 18 Disemba, 2013

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akihutubia wakati wa mkutano wake na wenyeviti wa Kamati za wakulima wa mwani za Mikoa miwili ya Pemba katika mkutano uliofanyika Ikulu mjini Chakechake Pemba tarehe 19 Disemba, 2013

Msikatishwe tamaa na bei ya Mwani

Wakulima wa mwani kisiwani Pemba wameiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa Mke wa Rais wa Zanzizbar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein na Mke wa Makamo wa pili wa Rais Mama Asha Suleiman Iddi kuharakisha kutekeleza mpango wake wa kuongeza thamani zao la mwani ili wakulima wa zao hilo waweze kunafika zaidi kutokana na kilimo hicho.

Ombi hilo limetolewa na wajumbe wa Kamati ya Mwani kutoka vijiji mbali mbali Pemba vyenye kulima zao hilo wakati walipokutana na Mke wa Rais wa Zanzibar mama Mwanamwema Shein na Mama Asha Suleiman Iddi katika ziara yake kisiwani Pemba na kufanya mazungumzo na kamati hiyo huko katika ukumbi wa Ikulu Chake chake Pemba.

Katika mipango yake, serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sekta binafsi, itaanzisha mchakato wa kujenga viwanda vinavyotumia malighafi inayopatikana hapa nchini hususan viwanda vya nguo, samaki, sukari, viwanda vya kuunganisha mitambo ya aina mbali mbali na vya kusindika mazao ya kilimo na matunda ili kuyaongezea thamani katika soko na kukuza uchumi.

Akitoa ufafanuzi kuhusiana na maombi ya wajumbe waKamati hiyo, Katibu Mkuu wa wizara ya Mifugo na Uvuvi Dk. Kassim Gharib amesema kuwa Serikali imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali katika jitihada zake za kulitafutia ufumbuzi suala la bei ndogo ya mwani kwa wakulima ili kuhakikisha kuwa nao wananufaika kutokana na kilimo hicho.

Miongoni mwa jitihada zinazochukuliwa na serikali ni pamoja na kutafuta matajiri wengine wa kununulia mwani kwa lengo la kuongeza ushindani wa ununuzi wa zao hilo. Jitihada nyengine ni kujenga kiwanda cha kusarifu mwani ambapo kwa sasa mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Korea na kwamba mtazamo wa serikali ni kujenga kiwanda hicho Kisiwani Pemba.

"Napenda nikuhakikishieni kwamba Serikali yenu ya Mapinduzi ya Zanzibar inalielewa vyema tatizo hili na juhudi zinaendelea za kulitafutia ufumbuzi" alisema Dk. Kassim Gharib.

Amezipongeza Kamati za mwani za Wilaya kwa juhudi kubwa zinazozichukua siyo tu katika kutatua migogoro ambayo hujitokeza katika maeneo yao, lakini pia katika kuzalisha kiasi kikubwa cha mwani licha ya changamoto mbali mbali zinazokikabili kilimo hicho. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya tani 15,000 za mwani zinazozalishwa hapa Zanzibar, asilimia 80 ya mwani huo unazalishwa Kisiwani Pemba.

Utafiti wa kitaalamu umeonesha kuwa zao la mwani linaweza kutumika kwa matumizi tofauti iwapo litasarifiwa na hivyo kuongeza thamani ya zao hilo kwa wakulima na watumiaji.

Katika taarifa yao kwa wake wa viongozi, wakulima wa zao hilo wamesema kuwa gharama za vifaa vya mwani zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku wakati bei ya zao hilo ya shilingi mia tisa 900 kwa kilo ya mwani mnene na shilingi mia nne 400 kwa aina nyengine ya mwani imekuwa haibadiliki licha ya ukweli kwamba bei hiyo ni ndogo sana na imekuwa haikidhi hata nusu ya gharama wanazozitumia. Hali hiyo imekuwa likiwavunja moyo wa kuendelea na kazi hiyo, ambayo wamesema iwapo itashughulikiwa inaweza kuwasaidia sana kuondokana na tatizo la ajira na umasikini wa jumla.

Bwana Faki Khamais Faki mkaazi wa Jimbo la Mgogoni shehia ya Mtemani amesema kuwa bado hakujawa na soko la uhakika la Mwani ambalo linawapa matumaini wakulima kutokana na matajiri wanaonunua mwani huo kutokuwa na utaratibu wa kupandisha bei jambo ambalo limekuwa likiwarejesha nyuma na kuendelea kuwaumiza.

"Tunaiomba Serikali iharakishe mpango wake wa kutafuta uwezekano wa kuanzisha kiwanda cha kusarifia mwani kwani hiyo ndiyo njia pekee itakayoondosha matatizo ya wakulima wa mwani" alisema Bwana Faki.

Mjumbe mwengine wa Kamati hiyo Bwana Khamis Sheha Mwadini Mkaazi wa Tumbe, ameishauri Serikali kujenga

majengo ya uhakika ya kuhifadhia mwani katika sehemu zinazozalishwa bidhaa hiyo kwa wingi kwa lengo la kuepuka kupata hasara hasa nyakati za mvua.

Amefahamisha kuwa sumu kubwa ya mwani ni kupata mvua, na inapotokea hali hiyo wakulima wengi huharibikiwa na mwani wao na hivyo kusababisha kupata hasara kwani hulazimika kuuza mwani wao kwa bei ndogo zaidi.

Nae Bi Hadia Mwinyi Soud Mkaazi wa Micheweni amesema kuwa wakulima wa mwani ni jeshi la baharini linalopigania uchumi kupitia zao la mwani lakini nguvu zao zinakuwa nyepesi kutokana na kukosekana kwa vifaa muhimu vya kuzalishia mwani. Hali inakuwa ngumu zaidi pale inapotokezea wakulima hao kupata ajali wanapokuwa baharini.

Mwanamwema Shein ambae ni mlezi wa Kamati hiyo na Mke wa Makamo wa pili wa Rais mama Asha Suleiman Iddi wamezipongeza kamati hizo kwa kufanyakazi katika mazingira magumu. Wamewasihi wakulima hao wasivunjike moyo kwani Serikali inatambua matatizo yanayowakabili na itaendelea kuyatafutia ufumbuzi hatua kwa hatua ili kuona shughuli zao hizo zinawaletea faida.

Viongozi hao wamesema watakuwa na utaratibu wa kufanya ziara maalum ya kuvitembelea vikundi vya uzalishaji wa mwani ili kukaa nao pamoja kuzungumzia masuala ya vikundi vyao na namna ya kuweza kuvisaidia.

SMZ itaendelea kuwasaidia vijana – Mama Shein

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein amesema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taasisi nyengine zitaendelea na juhudi zao za kusaidia vijana wanaoishi katika nyumba za kubadilisha tabia (Sobber Haouse) zilizopo Unguja na Pemba kwa lengo la kuwanusuru vijana kujiingiza katika vitendo viovu ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya.

Amesema kuwa Serikali, wafadhili pamoja taasisi mbali mbali zitaendelea kufanya hivyo kwa kuamini kwamba wao ni rasilimali muhimu ya taifa na ni tegemeo kwa familia zao.

Mama Mwanamwema Shein ameyaeleza hayo wakati alipokuwa akizungumza na vijana wanaoishi katika nyumba za kubadilishia tabia – "Sobber House" zilizoko Mkoroshoni Chake chake, Wete na Mkoani Pemba.

Amesema vijana wanaoishi katika nyumba hizo ni sawa na vijana wengine hivyo juhudi za makusudi zitaendelea kuchukuliwa kuyatafutia ufumbuzi matatizo yanayowakabili hatua kwa hatua.

Hata hivyo, Mama Mwanamwema Shein ameipongeza Jumuiya inayotoa elimu kwa jamii kuhusiana na athari za dawa za kulevya, ukimwi na mimba katika umri mdogo (JUKAMKUM) kutokana na juhudi wanazozifanya za utoaji wa elimu kwa vijana, shughuli ambayo imekuwa ikisaidia kuwanusuru vijana kutokana na majanga yenye athari kubwa kwa maisha yao.

Mama Shein ambaye katika ziara yake hiyo alifuatana na Mke wa Makamo wa Pili wa Rais Mama Asha Suleiman Iddi na Mke wa Balozi mdogo wa China mama Wu Yan pamoja na baadhi ya wake wa wabunge na wawakilishi kutoka Unguja, ametumia fursa ya ziara yake hiyo kuwahamasisha akinamama kuanzisha miradi ya maendeleo na kuweza kupambana na umasikini.

Akisoma risala yao kwa mama Mwanamwema Shein, Mratibu wa jumuia hiyo Bwana Hafidh Abdi Said amesema lengo la kuanzishwa jumuia hiyo ni kupunguza utumiaji wa dawa za kulevya, sambamba na kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi na ukimwi wenyewe. Aidha, Jumuiya hiyo imelenga kupunguza tatizo la watoto wa kike kupata mimba wakiwa katika umri mdogo na kupambana na maradhi nyemelezi ikiwemo kifua kikuu.

Katika jitihada za kufanikisha malengo yake, Jumuiya hiyo imeanzisha "dropping center" kwa lengo la kuwarahisishia vijana namna ya kujielewa na kuweza kujitambua wako wapi na wanahitaji kufikia wapi.

Nyumba hizo za kubadilishia tabia zilizoko Chake, Wete na Mkoani zimeweza kuchukua vijana wengi ambao baadhi yao wamerudi mitaani na kuwa tegemeo kwa familia zao na jamii kwa jumla.

Kituo hicho cha kunusuru vijana tokea kuanzishwa kwake mwaka 2010 kimeshapokea vijana 141, ambapo kati yao vijana 51 wanaendelea vizuri, 80 wamerudia matumizi ya dawa, 10 wameacha kabisa matumizi ya dawa za kulevya lakini wanatumia aina nyengine ya ulevi. Imeelezwa na Jumuiya hiyo kuwa hatua hiyo ni nzuri na inatia matumaini makubwa kwamba nyumba hizo zinaweza kusaidia kupunguza matumizi ya dawa za kulevya.

Mama Shein alikabidhi vifaa mbali mbali vikiwemo vyakula, mafuta, magodoro na vifaa vyengine kwa ajili ya matumizi ya vijana hao.

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein na Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mama Asha Balozi wakipewa maelezo kuhusiana na shughuli mbali mbali wanazofanya vijana walioamua kuacha matumizi ya dawa za kulevya Pemba tarehe 18 Disemba, 2013

Maadhimisho

ya siku ya UKIMWI Zanzibar

Tarehe 01Disemba ya kila mwaka duniani kote huadhimishwa siku ya UKIMWI. Hapa Zanzibar maadhimisho hayo mwaka huu yalifanyika kitaifa huko katika kijiji cha Paje, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja, ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa Mgeni Rasmi. Katika makala haya tunaelezea zaidi kuhusu maadhimisho hayo.

Ni maadhimisho ambayo mara nyingi huteka hisia za watu kutokana na historia na athari za ugonjwa huu kwa jamii. Kwa kawaida maadhimisho haya huambatana na utoaji wa elimu ya ugonjwa huu kwa njia mbali mbali ikiwemo sanaa kama vile maigizo, nyimbo, mashairi na ngonjera. Hapa ndio mara nyingi hadhara hutekwa na hisia na hata wengine kutokwa na machozi kutokana na ujumbe wanaoupata kutoka kwenye sanaa hizo.

Inawezekana kuwa maigizo hayo ndiyo yanayowaletea hisia hizo, lakini siyo jambo la kushangaza kuona kwamba maigizo hayo yanawakumbusha wapendwa wao ambao wameathirika na ugonjwa huo, hasa wale waliopoteza maisha. Hii inatokana na ukweli kwamba katika hali ya kawaida ya maisha ya zama hizi, ni vigumu au haiwezekani kukutana na familia ambayo haijaathirika kwa namna moja au nyingine na ugonjwa huu.
Hata hivyo, hali ya ugonjwa wa ukimwi sasa ni tofauti na zamani, ambako watu walikuwa wakitajiwa ugonjwa huu wanapatwa na hofu na mshituko mkubwa. Pamoja na hali hiyo, ukweli unabaki kuwa UKIMWI bado ni tishio kwa binadamu hasa kutokana na ukweli kwamba ugonjwa huu bado haujapata tiba.

Katika hotuba yake kwenye maadhimisho hayo, Rais wa Zanzibar na Mweneykiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisisitiza kuwa wazanzibari wasihadaiwe na takwimu za ugonjwa huo nchini kwa kuwa ugonjwa huu bado ni tatizo.

Aliwatahadharisha wazanzibari kutojenga dhana kuwa asilimia 1.0 ya watu wanaoishi na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI Zanzibar ni ndogo ikilinganishwa na nchi nyingine zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambako maambukizi katika nchi hizo kwa mujibu wa tafiti za mwaka 2011 yalikuwa ni asilimia 4.9.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia maonesho na shughuli za banda la kitengo shirikishi, Kifua Kikuu na Ukoma katika maadhimisho ya siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Kijiji cha Paje tarehe 01 Disemba, 2013.

Dk. Shein alinukuu matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya Ugonjwa wa UKIMWI na Malaria wa Mwaka 2012 (THMIS 3) ambayo yalionesha kuwa maambukizi ya ugonjwa huo Zanzibar yameongezeka kwa asilimia 0.4 kutoka asilimia 0.6 mwaka 2008 hadi asilimia 1.0 mwaka 2012.

Akifafanua hoja yake hiyo, Dk. Shein alieleza kuwa kwa mujibu wa takwimu za THMIS 3 na takwimu za Sensa ya Watu na Maakazi ya Mwaka 2012 ambazo zinaonesha kuwa Zanzibar ina wakaazi 1.3 milioni na asilimia 1.0 miongoni mwao wameambukizwa, maana yeke ni kwamba jumla ya watu 30,000 wanaishi na virusi vya ukimwi Zanzibar. Asilimia 69 ya kesi hizo ziko katika nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara. "Hakika hili si jambo la kuridhisha" anasema Dk. Shein na kuwataka wazanzibari kuwa waangalifu. Inakadiriwa kuwa Watu milioni 35 wameshaiaga dunia kutokana na ugonjwa huu.

Ametoa wito kwa wananchi wa Zanzibar kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali na taasisi za ndani na nje ya nchi kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya ugonjwa huo. Sambamba na wito huo akasisitiza wajibu wa kila mwananchi kushiriki katika kupiga vita unyanyapaa na ubaguzi wa aina yeyote ile dhidi ya waathirika wa ugonjwa huo ikiwa ni njia bora ya kuwatia moyo waathirika hao ili waweze kufaidika na jitihada mbalimbali zinazosaidia kupunguza nguvu za maradhi hayo.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alieleza hatua kadhaa ambazo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikizichukua katika vita dhidi ya Ugonjwa wa UKIMWI, ikiwa ni pamoja na kuanzisha kitengo cha kudhibiti ugonjwa huo katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mwaka 1986, mara tu baada ya dunia kubaini uwezekano wa kuenea kwa kasi kwa maradhi hayo duniani.

Katika mapambano dhidi ya UKIMWI Serikali imekuwa ikishirikiana na Jumuiya ya Kimataifa jambo ambalo lilipelekea kunaishwa Tume ya UKIMWI mwaka 2002. Miongoni mwa kazi za Tume hiyo ni kusimamia utekelezazji wa maazimio ya Shirika la Afya Duniani (WHO) la

kuzitaka nchi kuanzisha vyombo vya kitaifa vya kupambana na UKIMWI na magonjwa ya Uasherati.

Mbali ya kuunda Tume, mnamo mwaka 2005 Serikali ilianzisha vituo vya kutolea huduma za tiba kwa watu wenye VVU kwa kuanzia katika hospitali ya Mnazi Mmoja hadi sasa vituo hivyo vimeongezeka hadi kufikia 10 Unguja na Pemba.

Kwa upande wa Tume, imekuwa ikishirikiana na washirika mbalimbali katika mapambano dhidi ya UKIMWI na imeweza kupata mafanikio makubwa. Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Tume hiyo Zanzibar Profesa Saleh Mohamed Idrissa amesema kuwa Tume imepata mafanikio ya kupigiwa mfano katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kupanuka kwa shughuli za huduma na tiba kwa mujibu wa Mwongozo wa WHO kwa wenye virusi vya kiwango cha CD4 350 badala ya kile cha zamani cha CD4 200.

Alizidi kubainisha kuwa hadi Disemba 2012 asilimia 55 ya watu wanaoishi na VVU kwa kutumia kigezo cha CD4 chini ya 200 walikuwa wakipatiwa dawa wakati hadi Juni 2013 idadi ilifikia asilimia 63 kwa kutumia kiwango cha CD4 350.

Velevile Profesa Idrisa alieleza kuwa huduma za kupima kwa hiari zimeongezeka kutoka watu 86 mwaka 1986 hadi kufikia watu 87,326 mwaka 2012 ambapo kwa upande wa upimaji wa VVU kwa kina mama wajawazito kwa kipindi cha Januari hadi Septemba 2013 pekee jumla ya mama wajawazito 38,555 walipimwa katika vituo 151.

Ukiachia kueleza hatua hizo na mafanikio hayo, Dk. Shein aliweka bayana msimamo wa Serikali kuhusu azma yake ya kuendelea kuimarisha vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMIWI na kuimarisha huduma kwa watu wanaoishi na VVU.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kutekeleza Mpango Mkuu wa Afya na Mipango yetu Mikuu ya Maendeleo ikiwemo MKUZAII kwa sekta ya Afya ili kutimiza malengo yaliyowekwa ambayo yanajumuisha vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI" Dk. Shein alissiitiza.

Rais aliwahakikishia wananchi wa Zanzibar pamoja na washirika katika vita dhidi ya UKIMWI kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuongeza bajeti ya fedha katika miradi ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI kadri uwezo wa kifedha unavyoruhusu.

Aliwataka wananchi waliohudhuria maadhimisho hayo na wale waliokuwa wakifuatilia kupitia vyombo vya habari kuzingatia ujumbe wa mwaka huu wa maadhimisho hayo ambao ni kuondoa ziro tatu ifikapo mwaka 2015. Ziro hizo tatu ni kusiwepo maambukizi mapya, kusiwepo unyanyapaa, na kusiwepo vifo vinavyotokana na UKIMWI.

Inatia moyo kuona kuwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wameendelea kuonyesha ukomavu na kuikubali hali waliyonayo pamoja na masahibu yanayowapata. Wanastahiki kushukuriwa kwa moyo wao wa kutaka kuona jamii inaepukana na janga hili.

Katika salamu zao kwenye maadhimisho hayo waliipongeza Serikali kwa namna inavyofanya jitihada katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI pamoja na huduma inazozitowa kwa watu wenye VVU.

Walionyesha dhamira ya kufikia lengo la ziro tatu ifikapo mwaka 2015 na kuomba ushirikiano zaidi kutoka Serikalini, washirika katika mapambano dhidi ya UKIMWI na wanajamii.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake kuhusu athari za unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na VVU, Jumuiya hiyo nayo imeonesha wasiwasi wake kuhusu suala hilo ambalo imesema ni kikwazo katika kufikia lengo hilo.

Ni dhahiri kama walivyoeleza wanachama wa ZAPHA+ kuwa unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na VVU ndio adui mkubwa wa jitihada zinazochukuliwa na Serikali na washirika wengine walio katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Risala ya ZAPHA+ ilitahadharisha kuwa kwenye unyanyapaa na ubaguzi wanajamii hawawezi kujitokeza kupima afya zao. Katika hali hiyo inazidi kufafanua risala hiyo kuwa watu wanaoishi na VVU hawawezi kujitokeza si kwa tiba wala kupata huduma nyingine na hivyo kuongeza vifo ambavyo tumedhamiria kuvikomesha ifikapo mwaka 2015.

Kwa hiyo Dk. Shein aligeukia vitabu vya dini kueleza ubaya wa unyanyapaa na ubaguzi si kwa watu wenye VVU tu bali hata magonjwa mengine. Alieleza kuwa vitendo vya unyanyapaa na ubaguzi ni kinyume na haki za binadamu na Mwenyezi Mungu hapendezwi na vitendo hivyo.

Dk. Shein aliwakumbusha wananchi kuwa kuzingatia maadili mema na kufungamana na mafundisho ya dini pamoja na utamaduni wa nchi ni moja ya njia maridhawa ambayo inaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa katika jitihada za kupambana dhidi ya maambukizi mapya VVU.

"Tukumbuke kuwa dini na utamaduni wetu ni hazina kubwa katika kukabiliana na mtihani kama huu ndani ya jamii" alieleza Dk. Shein na kusisitiza kuwa dini zote zinahimiza uadilifu, tabia njema na kuwaasa waumini kujiepusha na mambo ambayo yanaathiri maisha yao.

Alitumia fursa hiyo kuwapa moyo na kuwanasihi watu wanaoishi na VVU kuendelea kufuata ushauri wa madaktari wakati wote ikiwemo kuendelea kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU maarufu ARV. Sambamba na nasaha hizo aliwataka wasikate tamaa na waendelee kuishi maisha yao ya kawaida ikiwemo kufanya shughuli zao za maendeleo.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi ZAPHA + Bibi Consolata John katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika Kijiji cha Paje tarehe 01 Disemba, 2013

Tangi la Maji safi na salama liliopo Gombani Wilaya ya Chake chake Pemba linalojengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika ADB

Jitihada za SMZ kuhusiana na suala la Maji na Ardhi

Maji ni uhai na hasa maji safi na salama. Kwa kufahamu hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM ilidhamiria kuchukua juhudi maalum kutekeleza mambo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kusambaza huduma ya maji safi na salama kutoka asilimia 75 mwaka 2010 hadi asiimia 95 mwaka 2015 mjini na kusimamia huduma hiyo kutoka asilimia 60 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2015 vijijini kupitia mradi mkubwa wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), ambao utajenga miundombinu ya maji Unguja na Pemba.

Katika kipindi cha miaka mitatu, Serikali imezingatia umuhimu wa huduma ya uhakika ya maji safi na salama katika Vijiji mbali mbali Unguja na Pemba. Usambazaji wa maji safi na usafi wa Mazingira unafanywa kwa kupitia Mradi wa Maji na Mazingira unaofadhiliwa kwa pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Makaazi (UN-Habitat), Serikali na Jamii. Mradi huu unahusisha kuchimba visima, kujenga matangi, kulaza mabomba, kujenga vyoo maskulini pamoja na kuimarisha vianzio vya maji.

Katika kutekeleza mradi huo, Serikali inaendeleza kazi za ujenzi wa miundombinu ya maji katika Miji mitatu ya Pemba na Vijijini Unguja na Pemba, sambamba na ujenzi wa matangi ya majaribio ya uvunaji wa maji ya mvua.
Kupitia Programu hii, Serikali imekamilisha Mradi wa maji Mkoa wa Mjini Magharibi awamu ya pili chini kwa ufadhili wa Serikali ya Japan kwa kujenga matangi makubwa mawili, uchimbaji wa visima vitano pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 21.

Kuhusu Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar (Zanzibar Water Supply and Sanitation Project) unaoendeshwa kwa mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, utekelezaji wake unaendelea vizuri. Kwa upande wa Unguja vijijini ujenzi wa matangi ya Matemwe na Nungwi umekamilika. Kwa upande wa Pemba vijijini kazi za Mradi zimekamilika kwa asilimia 87.64 na utekelezaji halisi umefikia asilimia 66.80.

Kwa upande wa Pemba Mijini ujenzi umefikia asilimia 54.17 na utekelezaji halisi umefikia 20.12 na visima vyote 10 vya uchunguzi wa maji tayari vimeshachimbwa kwa ajili ya miji yote mitatu ya Pemba. Kadhalika, kazi za uchimbaji msingi na ufungaji mabomba kwa maeneo yote ya Miji ya Wete, Chake Chake na Mkoani tayari zimefanyika kwa masafa ya km 12 kati ya 62.50 za mabomba kwa maeneo yote.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Balozi wa Finland nchini Tanzania Bibi Sinnika Antilia wakibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa kazi za usajili wa ardhi Zanzibar, kupitia mradi wa SMOLE unaofadhiliwa na Serikali ya Finland, katika sherehe iliyofanyika kwenye viwanja vya bustani ya Victoria "Victoria Garden" tarehe 23 Machi, 2013

Katika kuimarisha huduma za maji, Serikali ya Ras Al Khaimah inaisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchimba visima vya maji 50 kwenye maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Visima hivi tayari vimeanza kuchimbwa kwenye maeneo mbali mbali. Jumla ya visima 21 kati ya 50 vilikuwa vimeshachimbwa katika maeneo 14 ya Mkoa wa Mjini Magharibi na maeneo 5 ya Mkoa wa Kusini Unguja.

Pamoja na juhudi kubwa ambazo Serikali inazichukua katika kuziimarisha huduma za kupatikana maji safi na salama, sekta ya maji inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa maji chini ya ardhi na kwenye chemchem. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein mwenyewe ameshuhudia upungufu mkubwa wa maji wakati alipotembea vianzio vya maji Welezo, Saateni, Mwanyanya na maeneo mengine.

Hali ya uzalishaji wa chemchem karibu zote ikiwemo ya Mwanyanya na Mtopepo katika Mkoa wa Mjini Magharibi siyo nzuri sana. Wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi wanahudumiwa na visima 60 na chemchem 2. Kati ya visima hivyo, jumla ya visima 26 vipo Wilaya ya Mjini na visima 34 vipo Wilaya ya Magharibi. Upatikanaji wa maji kutoka katika chemchem za Mtoni na Mwanyanya zinazopeleka maji Mji Mkongwe ilikuwa ni zaidi ya asilimia 30 ya mahitaji ya Mkoa. Lakini kiwango cha kupatikana maji kimepungua kwa asilimia chini ya 15.

Tatizo kubwa lililopelekea kupungua kiwango cha maji ni uharibifu wa mazingira, ukataji wa miti kwenye maeneo hayo, wananchi kuyavamia maeneo hayo na kujenga kwenye vyanzo vya maji au kwenye uoto wa asili. Vile vile, kutokuwepo vivuli vya asili na mabadiliko ya tabia nchi, kunapelekea maji kukauka.

Rais wa Zanzibar ametoa wito kwa wananchi wasiyaharibu mazingira na wasiyavamie maeneo ya vyanzio vya maji, seuze kujenga kwenye maeneo hayo.

Kuhusu suala zima la matumizi endelevu ya ardhi, Serikali imeanzisha Idara ya Mipango Miji na Vijiji ambayo kazi yake kubwa ni kufanya mabadilko makubwa katika sekta ya ardhi (Land Reform).

Idara imeshapitia Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi wa mwaka 1995 na imeandaa Mpango Mkuu wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (National Land Use, 2013) ambao utawasilishwa Serikalini kabla ya mwezi wa Disemba 2013. Vile vile, mipango ya matumzi ya ardhi kimikoa imetayarishwa.

Kazi ya kutengeneza "Zanzibar Town Master Plan" imeanza rasmi tarehe 2 Mei 2013 na itamalizika Julai 2014 na kazi za Mikoa ya Unguja na Pemba nazo zimeanza na ile mipango midogo midogo ya vijiji inaendelezwa. Matumizi ya ardhi ya kijiji cha Nungwi tayari umefikia hatua za mwisho na utakuwa tayari mwisho wa mwaka huu wa 2013.

Serikali inaendelea na juhudi za kuweka mkakati wa matumizi ya ardhi (National Spatial Developement Strategy) kwa kutambua kuwa udogo wa ardhi ya Zanzibar, ifikapo 2014 na migongano ya kisekta katika kutumia ardhi. Maeneo yote muhimu na matumizi yake yatapangwa katika mkakati huu.

Serikali itatoa kipaumbele katika kufanya tafiti kwa ajili ya kuandaa makaazi bora na kuhimiza ujenzi wa nyumba za ghorofa. Utafiti wa ujenzi mpya wa eneo la Ng' ambo na ujenzi wa nyumba za ghorofa Ng' ambo utaanza mwezi wa Novemba 2013. Lengo ni kufikia azma ya Serikali ya A wamu ya Saba kuhakisha kuwa Wazanzibari wanapata makaazi bora.

Kuhusu viwanja kwa ajili ya ujenzi, jumla ya viwanja 1393 vimegaiwa kutoka mwaka 2010 hadi Septemba 2013 kwa ajili ya ujenzi wa aina mbali mbali.

Mafanikio ya Serikali katika sekta ya Miundombinu

Serikali imeweza kutekeleza vyema Ilani ya CCM ya mwaka 2010/2015, Dira 2020 na MKUZA II katika sekta ya miundombinu kwa kuzijenga barabara mpya kama ilivyokuwa imeahidiwa kwenye ilani hiyo. Kadhalika imeweza kuzifanyia matengenezo makubwa barabara mbali mbali za mijini na mashamba, Unguja na Pemba sambamba na kuimarisha huduma za umeme mjini na vijijini.

Ujenzi wa barabara ya Gando-Wete, Konde-Wete unaendelea vizuri na barabara za Kaskazini Pemba zinazojengwa kwa msaada wa MCC ambazo ni Bahanasa-Mtambwe, Mzambarautakao-Pandani-Finya, Mzambarau Karima-Mapofu, Chwale-Kojani na Kipangani-Kangagani, zenye urefu wa km. 35; nazo zimekamilika. Ujenzi wa barabara mpya ya Jendele-Cheju hadi Unguja Ukuu Kae Bona, tayari umeanza na ile ya Jumbi-Koani karibu itaanza.

Vile vile, Serikali imefanya jitihada za kuziimarisha huduma za bandari nchini na kwa kushirikiana na Kampuni ya Azam Marine imejenga upya majengo ya kuwahudumia abiria katika bandari ya Malindi. Kuna mpango pia wa kujenga jengo jingine la abiria bandarini hapo. Halikadhalika,upembuzi yakinifu umeshafanyika kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri na bandari ya Mkokotoni Unguja.

Serikali imeshughulikia vizuri ujenzi wa jengo jipya la abiria katika uwanja ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ambao umefikia hatua nzuri licha ya kujitokeza matatizo ya kiufundi ambayo tayari yamesawazishwa. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2014. Ujenzi wa eneo la kuegesha ndege (apron) na ujenzi wa barabara mpya ya kupitia ndege (taxiway) nao unatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Mafundi wa barabara wakiendelea na kazi za ujenzi wa barabara mpya Kisiwani Pemba.

Moja ya barabara zinazojengwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayokwenda katika kijiji cha Mtambwe Kisiwani Pemba

Ndani ya kipindi hiki cha miaka mitatu, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilianzishwa na imefanya marekebisho mbali mbali katika jengo la abiria na eneo la uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume. Utoaji wa huduma katika viwanja vya Unguja na Pemba umeimarishwa na vifaa mbali mbali vya kuimarisha ulinzi na usalama zikiwemo mashine za uchunguzi na vifaa vya zimamoto vimewekwa.

Serikali imezingatia umuhimu wa kuziimarisha huduma za usafiri wa baharini kwa kulifanyia mabadiliko makubwa Shirika la Meli la Zanzibar ili liweze kujiendesha kwa faida na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi.

Katika kutekeleza azma hii, Serikali ilifanya uamuzi wa kununua meli mpya. Hivi sasa, Serikali imeshafunga mkataba na Kampuni ya Korea ya Kusini na tayari ujenzi wa meli hiyo umenza ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na mizigo tani 200. Meli hiyo inategemewa kufika nchini mwezi Juni, 2015 na kusafirisha abiria na mizigo katika bandari za Unguja Pemba, Tanga na Da es Salaam.

Vile vile, matayarisho ya kutaka kununua meli mpya ya mafuta yenye uwezo wa kuchukua tani 3,500 tayari yameanza. Mkataba wa makubaliano unategemewa kufungwa kabla ya kumalizika mwaka huu na meli hiyo inategemewa kujengwa kwa muda wa miezi 18 baada ya kufungwa mkataba na inatarajiwa kufika nchini mwezi wa Juni hadi Agosti 2015.

Serikali inaendelea na hatua ya kusimamia taasisi zote zinazotoa huduma za mawasiliano ya simu kwa kupunguza idadi ya minara ya mawasiliano kwa Unguja na Pemba. Aidha, Serikali inasimamia mradi mkubwa wa mawasiliano ya "e-government" ambao unatekelezwa kwa awamu ya pili.

Tayari taasisi kadhaa zimeanza kutumia mtandao huo zikiwemo Bodi ya Mapato (ZRB), Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kituo maalum cha mawasiliano hayo.

Kuhusu suala la umeme, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imeitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha upatikanaji wa huduma za nishati ya umeme. Mradi wa ujenzi wa njia ya pili ya umeme kwa ajili ya Kisiwa cha Unguja wenye Megawati 100 uliojengwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani kupitia Shirika la MCC, umekamilika kwa wakati na ulizinduliwa rasmi tarehe 10 Aprili, 2013.

Kadhalika, mradi wa usambazaji wa umeme ulizinduliwa tarehe 11 Juni, 2013 ambao ulifadhiliwa na Serikali ya Japan. Mradi huo wa uimarishaji wa njia na miundombinu ya umeme umejumuisha ujenzi wa njia za kusambaza umeme kuanzia Mtoni hadi Tunguu, Mtoni hadi Fumba na Mtoni hadi Mahonda pamoja na Ujenzi wa Vituo vya kusambaza umeme huko Mtoni, Welezo na Mwanyanya.

Katika juhudi za Serikali za kusambaza huduma za umeme kwa wananchi, jumla ya Vijiji 110 vimefanikiwa kusambaziwa umeme katika miaka mitatu, kuanzia 2011 hadi 2013. Kati ya vijiji hivyo, vijiji 65 vipo Unguja na vijiji 45 Pemba. Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini hadi sasa umefikia asilimia 87.5 ya vijiji vyote vya Unguja na Pemba.

Serikali imechukua juhudi kubwa za kufanikisha mpango wa upatikanaji wa umeme mbadala na inaendelea kupata mashirikiano mazuri na Jumuiya ya nchi za Ulaya katika kutafuta njia mbadala itakayofaa ya kuzalisha umeme kwa njia ya Upepo au Jua. Mtaalamu tayari ameteuliwa na yupo nchini kwa maandalizi ya kufanyika uchambuzi yakinifu.

Wanafunzi wanaojifunza ushoni katika chuo cha kujifundisha ushoni Magomeni

Elimu ya amali ni ukombozi kwa vijana waliokosa kuendelea na masomo

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa umoja wa kitaifa imepata mafanikio makubwa katika jitihada zake ya kuimarisha elimu ya amali na mafunzo ya ufundi hasa kwa vijana waliokosa fursa ya kuendelea na masomo nchini.

Mafanikio hayo yana yanabainika kutokana na mwamko mkubwa wa vijana waliokosa kuendelea na masomo na kuamua kujiunga katika taasisi zinazotoa mafunzo mbali mbali ya amali na ufundi Unguja na Pemba.

Taasisi hizo ni zile zilizoanzishwa na Serikali ikiwemo Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, vituo vya Mafunzo vya Amali vya Mwanakwerekwe na Mkokotoni kwa Unguja na Vitongoji kwa Pemba. Kadhalika, kuna vituo vinavyomilikiwa na taasisi ya Serikali kama vile Skuli ya Mafunzo ya Amali ya Forodhani, iliyo chini ya Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima, Skuli ya Ufundi ya Mtoni inayomolikiwa na Jeshi la Kujenga uchumi na nyenginezo.

Vile vile , vipo vituo vya masomo ya aina hii vinavyomilikiwa na watu binafsi; mfano mzuri ni Chuo maarufu kinachotoa mafunzo ya ushoni Magomeni ambacho kimekuwa kimbilio kubwa la wananchi wa Zanzibar hasa akina mama walioamua kujiajiri wenyewe. Chuo hiki cha Zanzibar Modern Tailoring kinatoa mafunzo ya mishono ya nguo za aina mbali mbali. Chuo kingine cha aina hii kipo Chumbuni ambacho pamoja na masuala ya ushoni kinatoa pia mafunzo umeme, kompyuta, uashi na fani nyengine tofauti za ufundi.

Ni jambo la kutia moyo kuona kuwa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukabiliana na tatizo la ajira hasa kwa vijana linapata ufumbuzi kwa vijana wengi wanaomaliza masomo yao kujielekeza katika kupata mafunzo ya amali na tayari baadhi yao wameanza kujiajiri wenyewe. Jitahada za Serikali katika kuimarisha mafunzo yanayotolewa na taasisi inazozimiliki ni pamoja na kuyaimarisha mazingira ya taasisi hizo kwa kuwepo na mitaala iliyo bora, vifaa vya kufundishia, mazoezi na kutafuta walimu walio bora pamoja na kuwasaidia mipango na kupata mitaji na nyenzo za kuanzishia shughuli zao baada ya kumaliza mafunzo yao.

Akizungumza na Jarida la Ikulu, mkuu wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Bwana Abdulhamid Idrissa Haji amesema kuwa taasisi hiyo ambayo imeimarishwa zaidi katika uongozi huu wa Serikali ya Awamu ya Saba, imepata mafanikio makubwa kiutendaji. Amesema taasisi hiyo hivi sasa inatoa mafunzo ya uhandisi katika ngazi ya stashahada (NTA6). Mafunzo hayo yanajumuisha uhandisi wa mitambo, uhandisi wa magari, uhandisi wa ujenzi na usafirishaji, uhandisi mawasiliano ya anga, eletrinoki na Kompyuta na uhandisi wa umeme.

Amesema kuwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Taasisi hiyo imeongezeka kutoka wanafunzi 237 mwaka 2010 hadi kufikia wanafunzi 1,215 mwaka 2012/2013. Kwa upande wa masomo ya kujiendeleza ya ufundi stadi, stashahada ya ICT, mafunzo ya Hesabati na elimu ya msingi na kidato cha nne, taasisi hiyo ina jumla ya wanafunzi 99.

Majengo ya Chuo cha mafunzo ya amali - Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Bibi Khadija Omar Said ambaye Mamlaka anayoiongoza ndiyo inayosimamia vituo vya mafunzo ya amali vya Mwanakwerekwe, Mkokotoni na Vitongoji, ameliambia Jarida la Ikulu kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana wanaojiunga na vituo hivyo kwa kusoma masomo ya amali na ufundi yanayojumuisha ufundi wa umeme, useremala, ushoni, ufundi magari, kompyta na mengineyo. Idadi ya vijana katika vituo hivi imeongezaka kutoka wanafunzi 435 mwaka 2010 mpaka 704 mwaka 2013. Tayari vituo hivi vimeshatoa wahitimu 50 wa fani mbali mbali.

Mamlaka hii hivi sasa ina mipango ya kujenga vituo vipya vya mafunzo ya amali katika Mkoa wa Kusini Unguja, na Kaskazini Pemba. Kadhalika tayari maombi ya vituo binafsi vya mafunzo ya amali yapatayo 105 yamepokelewa kwa ajili ya kupata usajili. Baadhi ya wanafunzi wanaomaliza mafunzo katika taasisi hii wameanza kujiajiri wenyewe na wapo waliopata fursa ya ajira katika taasisi za Serikali na za binafsi.

Jarida la Ikulu lilipata fursa ya kuzungumza na kijana Hashim Moh' d Ibrahim wa Mwanakerekwe amabaye alipitia taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na baada ya kuishia na elimu yake ya kidato cha pili miaka minne (4) iliyopita. Kijana huyo alijiunga na mafunzo ya cheti fani ya ufundi wa kutengeneza mafriji na hivi sasa tayari amejiajiri mwenyewe.

" Baada ya miezi tisa nilikatisha mafunzo kwani nilishaanza kufanya kazi zangu katika eneo la Meli nne Mwanakwerekwe pahala ambapo nilikuwa nikifanya mazoezi ya vitendo. Motokeo ni mazuri, na sasa nimeshaanzisha eneo langu hili, ninao wasaidizi wangu watatu nao wanapata ujuzi na chochote" alimaliza huku akionesha kuridhika na mafanikio aliyoyapata kutokana na shuguli zake za kutengeneza mafriji na viponza hewa (Air Conditions), ambapo miongoni mwa wateja wake wakubwa ni wenye kumiliki hoteli mbali mbali za kitalii.

Mafanikio ya Kijana Hashim na wengine kama yeye, yanamthibitishia kila mtu kwamba kumbe ajira siyo ile tu inayotokana na kuajiriwa Serikalini, lakini vijana wanaweza kujiajiri wenyewe iwapo wataamua kujiunga na mafunzo ya amali kwenye vyuo ambavyo vimeenea katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

Wazazi na walezi hawana budi kuchangamkia fursa hizo ili waweze kukabiliana vyema na tatizo la ajira hasa kwa vijana. Vijana nao wanapaswa kuzitumia fursa zilizopo za mikopo katika mabenki pamoja na huduma zinazotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia taasisi zake ikiwemo Wizara ya Nchi, Kazi na Utumishi wa Umma na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Wanafunzi wa Taasisi ya Ufundi na Sayansi na Teknologia Karume wakiwa darasani wakijifunza masomo ya uhandisi kwa vitendo

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipewa maelezo na mtaalamu wa kuweka nyasi bandia katika uwanja wa Amaan wakati alipotembelea kuona maendeleo ya kazi hiyo tarehe 6 Oktoba, 2013

Sekta ya Habari,

Utamaduni na Michezo zimeimarika zaidi

Suala kuhusu haki ya wananchi kupewa taarifa wakati wote kuhusiana na matukio mbali mbali yanayotokea nchini na duniani kote na ambayo ni muhimu katika harakati zao za maisha pamoja na shughuli zao za kila siku, ni suala la kikatiba ambalo Serikali inalazimika kuhakikisha kuwa linatekelezwa.

Imeelezwa ndani ya katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 18 (2) kwamba "Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii".

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 nayo inaielekeza Serikali kusimamia utekelezaji wa Sera ya Habari na kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari nchini. Katika kutekeleza agizo hili, Serikali katika kipindi cha miaka mitatu imetoa vibali vya kuanzishwa Redio nne (4) za FM na Televisheni tano (5). Sambamba na hatua hizo, Shirika la Magazeti ya Serikali limeweza kuwafikia wasomaji wengi zaidi kwa kuongeza maeneo ya usambazaji Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

Katika kipindi hiki Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) lilianzishwa na Serikali na ililazimika kuchukua hatua kadhaa, kama vile kununua vifaa na mitambo ya kisasa, ili viweze kurusha matangazo yake kwa ufanisi, kuonekana na kusikika katika sehemu mbali mbali ndani na nje ya Zanzibar. Katika kipindi hiki Serikali ilifanya uamuzi wa kuingia katika utaratibu wa kisasa wa digitali kwa kununua vifaa na mitambo mipya kwa ajili ya kuimarisha shughuli za utangazaji Zanzibar.

Mafunzo ya kuwaendeleza wanahabari mbali mbali yalitolewa kwa lengo la kuyatekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Katika kipindi cha miaka mitatu, jumla ya waandishi 38 wameweza kupatiwa mafunzo katika viwango vya stashahada, shahada ya kwanza na shahada ya pili.

Vile vile, Serikali iliyaimarisha matangazo ya redio kwa kuuhamisha mnara wa masafa ya kati (medium waves) kutoka Chumbuni na kuupeleka Bungi, ambako Ofisi na Studio mpya na nyumba mbili (2) za kisasa za familia nne za wafanyakazi zimejengwa. Aidha, ukarabati wa mnara wa mawimbi mafupi (short wave) nao umefanyika. Ukarabati huo umefanywa kwa ushirikiano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Chuo cha Uandishi wa Habari nacho kimeimarishwa kwa lengo la kujitosheleza kwa wanahabari. Vifaa vya kufundishia vilinunuliwa na walimu wenye ujuzi waliajiriwa. Katika kuimarika kwa chuo hicho, hivi sasa wanafunzi wanaosomea cheti na stashahada wameongezeka kutoka 75 mwaka 2009/2010 hadi kufikia 122 kwa mwaka 2010/2011.

Kwa upande mwingine, Serikali imelishughulikia tatizo la uingizaji wa vifaa vya utangazaji vya TV na redio vilivyopitwa na wakati, ili kuepusha Zanzibar kugeuzwa kuwa jaa. Serikali ilitekeleza kwa mafanikio makubwa Mkakati wa Mageuzi ya Teknolojia ya Utangazaji kutoka analogi kwenda dijitali.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwaangalia watoto wakicheza ngoma ya kibati katika Tamasha la Utamaduni la Urithi wa Mangapwani Wilaya ya Kaskazini B Unguja

Vile vile, jengo la Utangazaji la zamani liliopo Rahaleo limefanyiwa matengenezo mkubwa ili liweze kutumika kwa ajili ya studio za kurikodia nyimbo za wasanii wa Zanzibar. Hivi sasa Serikali tayari imeshachukua hatua ya kununua vifaa vya studio hiyo.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Serikali imechukua hatua za kuifanyia mapitio na marekebisho Sera ya Utamaduni na Michezo na sheria zinazoongoza taasisi zinazosimamia utamaduni, ili ziweze kwenda sambamba na wakati ambapo utamaduni unajumuishwa katika dhana ya utalii kwa wote.

Katika kuufanya utamaduni uwe na tija zaidi, wizara imeweza kukamilisha mchoro wa ramani ya Utamaduni katika shehia za Unguja na Pemba, pamoja na Utafiti wa Urithi wa Utamaduni katika mikoa mitano ya Zanzibar ili hatimaye ihifadhiwe na itangazwe nchi za nje kwa kuingizwa katika orodha ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Say ansi na Utamaduni (UNESCO) ya tamaduni zinazohifadhiwa. Hivi sasa Serikali imo katika mchakato wa kuifanyia marekebisho makubwa sheria ya sanaa inayokusanya mambo yote ya utamaduni. Mswada huo wa sheria hivi sasa unaandaliwa.

Kuhusu ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha michezo na sherehe za kitaifa, Serikali imeuchagua uwanja wa Mao Tse Tung uliopo mjini Unguja utumike kwa shughuli hizo. Michoro ya awali tayari imeshakamilika na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imekubali kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ujenzi huo ambapo mkataba wa makubaliano tayari umetiwa saini na pande mbili hizo.

Uwanja wa Gombani Pemba tayari umefanyiwa marekebisho kwa kuweka nyasi bandia, hatua ambayo inaufanya uwanja huo kufikia kiwango cha kuchezwa mashindano ya kimataifa ya mpira wa miguu.

Kadhalika, matengenezo ya taa za uwanja huo yamekamilika ambayo yanauwezesha uwanja kutumika hata wakati wa usiku. Serikali hivi sasa imeanza utaratibu wa kuezeka paa jipya na ujenzi wa njia ya kukimbilia ili kutoa fursa ya michezo ya riadha kufanyika kulingana na viwango vya kimataifa. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, ujenzi wa kiwanja cha michezo ya ndani umeanza na unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Disemba 2013.

Kwa upande wa Uwanja wa Amaan, ukarabati mkubwa unafanyika kuimarisha eneo la kuchezea, ambapo nao utawekwa nyasi bandia kama ilivyo Gombani. Kazi hii inatarajiwa kukamilika katikati ya mwezi wa Disemba na utatumika kwa ajili ya mashindano ya maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Serikali imechukua hatua mbali mbali za kuzilinda, kuzihifadhi na kuzidumisha mila, silka na maadili mema ya Wazanzibari. Hatua zimechukuliwa za kuzikagua kazi za sanaa na kuchukuliwa hatua za kuilinda na kuhifadhi mila na silka kulingana na matokeo ya ukaguzi huo. Kukamilika kwa Kamusi la Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu kutapelekea wananchi kuyatumia makamusi hayo ili kuulinda utamaduni wa Mzanzibari.

Aidha, kumekuwa na uhakiki wa Matamasha, Matangazo ya kibiashara, Video za nyimbo, Tenzi zenye maudhui mbali mbali na Filamu tofauti katika maduka ya kukodishia kanda Unguja na Pemba. Bodi imekagua pia vikundi vya ngoma, michezo ya kuigiza jukwaani, tenzi na mashairi ya kughani ili kuhakikisha mila, silka na utamaduni wa Kizanzibari hauathiriwi.

Hatua hizo zinakwenda sambamba na hatua za kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria na mambo ya kale. Utafiti wa uchimbaji wa eneo la Ngome Kongwe, Forodhani Unguja kulingunduliwa vigae vya vyungu, 'Kwale pottery' vya karne ya kwanza. Aidha, matengenezo yamefanyika kwa jengo la makumbusho la Mahodhi ya Hamamni (Hamamni Baths) ili kulirudisha katika hadhi yake ya awali na kuweza kuongeza idadi ya vivutio kwa wageni. Serikali imeyafanyia matengenezo majengo ya Mangapwani kwenye mahandaki ya vita Kuu vya Pili vya Dunia pamoja na mnara wake na magofu ya Kizimbani, Hamamni na jengo la Beit el Ajaib.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatana na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi wakati alipokuwa akiangalia bwawa la ufugaji wa kasa huko Nungwi Wialaya ya Kaskazini A Unguja.

Maendeleo

ya sekta ya uvuvi na mifugo Zanzibar

Kwa kuzingatia maumbile na jiografia ya Zanzibar, uvuvi ni shughuli muhimu ya kiuchumi miongoni mwa wananchi wengi wanaoishi pembezoni mwa mwambao wa bahari. Lakini kutokana na ukosefu wa zana bora za uvuvi wa kisasa, wavuvi wengi hasa wadogo wadogo wamekuwa wakisababisha uharibifu wa mazingira kwa kuharibu matumbawe ambayo ndiyo mazalio ya samaki.

Ili kuimarisha uvuvi wa kisasa ambao ni endelevu na unaozingatia uhifadhi wa mazingira ya bahari na kukuza kipato cha wavuvi, Serikali kupitia ilani ya CCM, ilidhamiria kutekeleza mipango kadhaa ikiwemo mpango wa kuandaa sera ya uvuvi na kusimamia utekelezaji wa sheria ya uvuvi kwa lengo la kuimarisha uvuvi na uhifadhi wa mazingira ya bahari, sambamba na kuendelea kuwashajiisha wavuvi kuanzisha vikundi vya ushirika, matumizi ya maarifa ya zana za kisasa, na misaada au mikopo itakayowasaidia kununua zana hizo.

Aidha, kupitia ilani hiyo ya CCM, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilidhamiria kuendeleza uhifadhi wa viumbe hai na dimu vya baharini kama vile kasa, pomboo na vyenginevyo ambavyo vinaweza kutumika pia kama ni sehemu ya kivutio cha utalii.

Tathmini inaonesha kuwa Serikali tayari imefanikiwa vizuri katika kutekeleza ilani hiyo kwa upande wa kuimarisha sekta ya uvuvi na mazao ya baharini kutokana na mwamko mkubwa wa ufugaji wa samaki na uhifadhi wa viumbe vya baharini.

Kijiji cha Kizimkazi kimeendelea kupata umaarufu mkubwa kutokana na watalii wengi kwenda kuangalia samaki. Umaarufu kama huo pia umeendelea kukua katika kijiji cha Numngwi ambako wananchi wa kijiji hicho waliamua kuhifadhi kasa ambao utafiti wa kitaalamu wamebaini kuwa aina hiyo ya samaki inaendelea kutoweka duniani.

Katika siku za karibuni kijiji cha Jozani, ambacho kwa muda mrefu kilikuwa maarufu kwa kimapunju na msitu wa asili, sasa kimeanza kutembelewa na watalii wengi ambao wanakwenda kuangalia siyo kimapunju na msitu tu, lakini pia wanakwenda kuona kasa, makobe na mabwawa ya kufugia samaki ambayo

Moja kati ya mabwawa darasa ya ufugaji wa samaki Jozani, lililojengwa kwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Jumuiya ya Wenye Mashamba Jozani (UWEMAJO) na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

yamejengwa na Serikali na wanajamii kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, hasa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa – UNDP.

Sehemu kubwa ya huduma hizo zinatolewa na wanajamii ambao wameshajiika kuanzisha vikundi kwenye maeneo yao.

Katika kipindi cha miaka mitatu (3) tokea serikali ya awamu ya saba ilipoingia madarakani, juhudi mbali mbali zimechukuliwa katika kuiendeleza sekta ya uvuvi, ambayo mchango wake katika Pato la Taifa umepanda kutoka asilimia 6.1 mwaka 2011 hadi asilimia 6.7 mwaka 2012.

Kadhalika, kiwango cha samaki kilichovuliwa kimeongezeka kutoka wastani wa tani 26,600 mwaka 2010/2011 hadi wastani wa tani 30,500 mwaka 2012/2013. Uzalishaji wa mwani nao uliongezeka kutoka tani 12,500 mwaka 2010/2011 hadi kufikia tani 13,844 mwaka 2012/2013. Serikali ilifanya juhudi maalum ya kuwawezesha wavuvi kwa kuwapa mafunzo ya uvuvi bora unaozingatia uhifadhi wa mazingira pamoja na matumizi bora ya vifaa vya kisasa kupitia Mradi wa MACEMP, ambapo jumla ya Tsh. 4.86 bilioni zilitumika.

Kuhusu sekta ya ufugaji, Serikali imeandaa sera ya ufugaji katika kipindi hiki cha miaka mitatu na imeendeleza juhudi za kuwaendeleza wafugaji kupitia programu mbali mbali ikiwemo programu ya kuimarisha huduma za mifugo (ASDP-L). Jumla ya vikundi 335 vya Unguja na Pemba vilipewa mafunzo. Wafugaji 3,200 walitembelewa na kupewa ushauri. Vile vile, huduma za utafiti na utibabu wa wanyama ziliimarishwa na matengenezo ya Maabara ya Maruhubi na Chake Chake yalifanyika.

Kwa upande wa Mapinduzi ya Uvuvi, Serikali imeliangalia suala hilo kwa upana wake. Kimsingi, Mapinduzi ya Kilimo Zanzibar, hayaangalii tija na ubora wa mazao pekee, bali imeangalia suala la uhaba wa ardhi, ongezeko la idadi ya watu na kupanuka kwa shughuli mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika ardhi ambayo ukubwa wake hauongezeki.

Katika kufikia malengo yake, Serikali imefanya jitihada maalum kwenda kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi za nje kama vile China na Vietnam. Wavuvi na wakulima wa mwani 59 wamepelekwa nchini China kujifunza. Aidha, viongozi mbali mbali nao walifanya ziara ya kujifunza mambo ya uvuvi nchini China na Vietnam.

Katika kutekeleza dhamira ya kuimarisha taaluma ya ufugaji wa samaki, Serikali imeanzisha bwawa la mfano la kujifunza kufuga samaki Jozani na jengine litaanzishwa Donge hivi karibuni. Hivi sasa, shughuli za ufugaji wa samaki zinaendelea katika maeneo mbali mbali Pemba na zimeonesha mafanikio makubwa katika vijiji vya Muambe, Chambani, Pujini Kibaridi, Jadida, Kiungoni Wete, Makombeni, Chokocho na maeneo mengine.

Wataalamu wa masuala ya uvuvi wamethibitisha kuwa ufugaji wa samaki ni njia muafaka ya kuondoa umasikini katika jamii kutokana na urahisi wa kazi yenyewe ya kufuga hadi kufikia hatua ya kuvuna samaki.

"Kazi ya kufuga samaki ni rahisi, haihitaji zana kubwa kama zile zinazohitajika kwenda kuvua kwenye bahari kuu, lipo soko la uhakika na akinamama wengi wanaweza wakafanya kazi hii bila ya shida" alisema Dr. Nerman S. Jidawy, Mhadhiri wa Taasisi ya Elimu ya Sayansi ya Baharini - IMS ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Zanzibar.

Katika juhudi za kuimarisha uvuvi wa bahari kuu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetiliana saini mkataba wa Maelewano ya Awali (MoU) na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika masuali ya kuendeleza uvuvi.

Tudumishe Amani, Umoja na Maendeleo ambayo ni Matunda ya Mapinduzi yetu
SMZ
SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
50
MIAKA 50 YA MAPINDUZI
ZANZIBAR
1964 - 2014
UNGUJA
PEMBA
MAPINDUZI DAIMA